Naye alitoa wengine kuwa Mitume . . .

Fundisho la kina kuhusu karama tano zake Yesu Aliyepaa:

WAEFESO 4:11

Na Mtume Paulo Galligan

HUDUMA YA UVUVIO YA AUSTRALIA

YALIYOMO

UTANGULIZI: Naye Alitoa wengine kuwa Mitume, wengine kuwa Manabii, wengine kuwa Wainjilisti, wengine kuwa Wachungaji na Waalimu

SURA YA KWANZA: Huduma katika Utano katika Chuo cha Matendo ya Mitume

SURA YA PILI: Karama ya huduma ya Mtume

SURA YA YATU: Karama ya Huduma ya Nabii

SURA YA NNE: Karama ya Huduma ya Muinjilisti

SURA YA TANO: Karama ya Huduma ya Mchungaji

SURA YA SITA: Karama ya huduma ya Mwalimu

SURA YA SABA: Waefeso 4:7-16 Neema ya Kuufikia ukomavu

UTANGULIZI

Naye ndiye alwatoa wengine kuwa mitume, wengine kuwa manabii, wengine kuwa wainjilisti, wengine kuwa wachungaji na waalimu. Waefeso 4:11

LENGO NI KANISA LILILOKAMILIKA

Yesu Kristo anajiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu lisilo na mawaa. (**Efe.5:27**).
Analiandaa kanisa hili kwa kulitakasa na kuliosha kwa maji katika Neno (**Efe.5:26**).
Hili ndilo kanisa ambalo limekamilishwa (**Efe.4:11-16**).
Hili ni kanisa ambalo limefikilia ule ukamilifu (**Ebr.6:1-3**). Tunaufikia ule ukamilifu **"*Mungu akitujalia"***. Mungu anatutarajia tuwe na msingi ulio imara.
Kanisa hili linawakilishwa na wanawali watano wenye busara katika **Mathayo 25:1-13**. Hili kanisa tukufu, limetiwa mafuta kikamilifu na Roho Mtakatifu; taa zake zinaangaza sana katika ulimwengu uliojaa giza na utawala wa mpinga Kristo.
Hili ni kanisa linalofahamu siri ya Mwili wa Kristo (**Efe.3:6**), ambalo linajumuisha Myahudi na Myunani katika mwili mmoja (**Efe.2:14-16**).
Hili ni kanisa linalopokea hekima iliyofichwa ya Mungu (**1Kor.2:6-10**); ambalo limepokea ***"nia ya Kristo"*** (**1Kor.2:16**).

Kuna mafundisho mengi katika Maandiko Matakatifu juu ya Kanisa lililokomaa, kanisa linalo kaza mwendo kuufikilia utimilifu, maana hilo ndilo lengo la Mungu kwetu sisi.

YESU KRISTO ALITOA YOTE KWA AJILI YA KANISA

Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alipitia katika aibu akiwa katika mwili kama mwanadamu, ***"bali alijifanya kuwa hana utukufu"***, na kuteseka hata kufa, ***"hata mauti ya msalaba"*** (**Fil.2:7-8**), ili ajitwalie kanisa. Yeye ndiye Mwokozi wa ule Mwili (**Efe.5:23**). Hata **"*alishuka mpaka pande zilizo chini za nchi"*** (**Efe.4:8**-10) [hata kuzimu yenyewe **1Pet.3:18-19**] na kisha kupaa juu sana kupita mbingu zote, na kuteka mateka. Kupitia kushuka na kupaa Kwake, Yesu aliupata ushindi mkuu ambao ulibadilisha historia milele na kwa ajili ya kazi ya ukombozi Wake, Aliweza kupokeza kanisa **karama tano za huduma za Mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu**. Bila hizi karama, kanisa halingeweza kuufikilia ule utimilifu na ukamilifu. Kazi ya karama hizi tano za huduma ni kwa njia nyingi hujidhihirisha katika kuuukamilisha Mwili wa Kristo, ***"ambaye katika yeye mwili wote ukiungamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo."*** (**Efe.4:16**)
Huo mni mwili uliokamilika ambao BWANA anajenga ulimwenguni, na anafanya haya yote kwa kutoa wengine kuwa mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu.

MUNGU ANALIJENGA KANISA

Yesu alisema katika **Matt.16:18** ***"… Nitalijenga kanisa langu …"*** Mungu anajenga nyumba ama hekalu, tukitumia lugha ya Agano la Kale. Hekalu hili linajengwa kw mawe yaliyo hai; tunajengwa kuwa nyumba ya Roho ili Mungu akae ndani yake, ambamo sisi kama makuhani tunatoa dhabihu za Roho zinazokubaliwa na Mungu, (**1 Pet.2:5**). Jingo hili linajengwa kwa msingi wa mitume na manabii (**Efe.2:20,** & **1Kor.12:28**) Hizi ni huduma za msingi, mara nyingi hufanya kazi bila kuonekana wazi wazi. Bila mitume na manabii jingo halitaweza kujengwa. Ni ***'fundisho la mitume'*** ambalo kanisa linatakiwa kuitolea kwake (Matendo **2:42**).

Mitume wanaweka msingi, wanakuwa waangalizi wa jengo na hata kulikamilisha.

ZERUBBABELI NI MFANO WA MTUME

Zekaria Sura ya 4

Ili tukaweze kuelewa huduma ya mtume, twahitaji kujifunza kutoka kwa huduma ya Zerubabeli liwali wa jimbo la Yerusalemu na ambaye aliyeidhinishwa kulijenga hekalu la Mungu, wakati wa urejesho baada ya uhamisho wa Babeli.

aya.9*"Mikono yake Zerubabeli imeiweka misingi ya nyumba hii"*. Zerubabelui aliweka msingi kwa hivyo ni mfano wa mtume. Aya hii inaendelea kusema ***"na mikono yake ndiyo itakayoimaliza; nawe utajua ya kuwa BWANA wa majeshi amenituma kwenu."***

Hili linahusiana na hudumka ya mtume. Wakati Mungu anapomuinua mtume, Yeye humpa huyo mpangilio mkuu. Paulo anajizungumzia kama mjenzi stadi (**1Kor.3:10**); ya kwamba alipewa na Mungu mipango ya kulijenga kanisa. Paulo pia anatufunulia aina ya mipango mingi katika chuo cha **Waefeso**.

KUJENGWA KWA NGUVU ZA ROHO

aya.6 Inatupatia tafsiri ya maono ambaye BWANA alimwonyesha Zerubabeli, ***"Hili ndilo neon la BWANA kwa Zerubabeli, kusema, si kwa uwezo wala si kwa nguvu, bali ni kwa Roho yangu, asema BWANA wa majeshi."*** Hili ni neon la BWANA kwa mtu ambaye amekabithiwa jukumu la kujenga tena hekalu la Mungu. Kazi hii yaweza tu kutimizwa kwa upako wa Roho Mtakatifu. Neon la BWANA kwa Zerubabeli ni 'si kwa nguvu za mwanadamu wala uweza; si kwa nguvu za mwanadamu wala siasa'. **Ni kwa Roho Mtakatifu, kwa ufunuo, ni kwa njia ya upako wa Mungu ndio utakaowezesha kanisa hili kujengwa.**

KUJENGWA KWA NEEMA

Zerubabeli anapishwa na Mungu kwa njia ya nabii Hagai na nabii Zekaria, kujenga nyumba ya Mungu. Huyu ni mjenzi, mtume ambaye anaweka msingi, kujenga kuta na pia kuimalizia kuijenga kwa kelele kusema ***"neema, neema ilikalie!"*** Linajengwa kwa neema kwa njia ya imani wala sio kwa matendo mtu asdije akajivuna, ni karama ya Mungu. (**Efe.2:8-9**) na hii ni karama ya mtume ambaye Mungu amemfunulia mpangilio wa namna ya kulijenga kanisa la Mungu siku hizi za mwisho.

KUJENGWA KWA IMANI

v. 7 ***"Nani wewe, Ee mlima mkubwa? Mbele ya Zerubabeli utakuwa nchi tambarare!"***

Neno la Mungu lanena juu ya Zerubabeli, 'mlima ulio mbele yako utakuwa tambarare'.

Unabii huu pia unaonyesha kwamba mtume ana mamlaka ya kukabiliana na kila kizuizi la maksudi ya Mungu (**2Kor.10:3-6**).

Isa.40:4 akinena kuhusu huduma inayokuja ya Yohana Mbatizaji anasema ***"Kila bonde litajazwa na kila mlima na kilima," kwa ajili ya kuinyosha njia ya BWANA***.

Yesu alisema katika **Marko 11:23*"Amin, nawaambia, yeyote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba, hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake."* Kuwa na imani ya Mungu na utaing'oa milima. Na hii ndio imani itakayojenga kanisa.**

YESU NI MTUME WA MUNGU, ANAJENGA KANISA

Mikono ya Yule aliyeweka msingui wa hekalu ndiyo itakayo ikamilisha. (Zak.4:9)

Yesu ndiye aliyeweka msingi wa hekalu!

Yesu Kristo ndiye atakayekamilisha hii kazi!

Yesu analijenga kanisa kwa njia gani?
Kupitia kwa mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu ambao yeye mwenyewe amewatoa **Efe.4:11**. Wakati linapokamilika, kila mtu atasema, ***'hakika hili ni kanisa la Mungu aliyehai***. ***'Tazama jinzi lilivyo, ajabu, kanisa ulimwenguni kote, ambalo limeinuliwa kutoka kwa kila taifa, kila kabila, lugha na makundi ya watu.'***

aya.10*"Maana ni nani aliyedharau siku ya mambo madogo?* Kazi lazima ianze kwa kuweka msingi, na mambo madogo! Uvuvio wa Uingereza wa mwaka 1904-5 haukudumu pakubwa ka sababu ya ukosefu wa watenda kazi wenye ujuzi. Sehemu kubwa ya huduma ya mtume nyakati hizi ni kukuza watenda-kazi kwa ajili ya mavuno.

Maana hawa saba wanafurahi kutia timazi mkononi mwa Zerubabeli."
Hao 'saba' wanawakilisha Roho Mtakatifu. **Ufunuo 5:6** yatwambia kuwa macho saba ni Roho saba za Mungu. Yesu ndiye Mtiwamafuta ambaye alimpokea Roho Mtakatifu bila kipimo. Roho Mtakatifu anafurahia kuona timazi mkononi mwa Zerubabeli. Timazi hutumiwa kwa ajili ya kuchunguza unyofu wa ukuta. Ni kitu ambacho ni lazima tujipime. Lazima tujipime na Neno la Mungu. Timazi ni Neno la Mungu katika mikono ya Zerubabeli, mtume. Kanisa la siku hizi za mwisho ni lazima lijipime na Neno la Mungu. Wakati atu wa Mungu wanapojihukumu kwa Neno, na kuwa sawa na Maandiko Matakatifu, na wasipungukiwe na utukufu wa Mungu tena kwa ajili ya dhambi, basi Roho Mtakatifu anafurahia na kuwatia mafuta zaidi.

NABII
Nabii anafanyakazi bega kwa bega na mtume, huku akitia nguvu hiyo misingi, kwa kuliweka kanisa katika mpangilio mzuri. Huduma ya nabii ni kuliongoza kanisa hata lifikilie utimilifu. Nabii analeta ufunuo wa Neno la Mungu kwa kanisa. Wakati ambapo huduma ya mtume na nabii zinapokuwa zinafanya kazi pamoja, kanisa linakuwa na msingi dhabiti.

MUINJILISTI
Muinjilisti anaenda kuchimba migodi na kuchonga mawe mapya kwa ajili ya ujenzi wa kuta za nyumba ama kanisa. Muinjilisti ni huduma ya kwanza ya wazi. Kwa hivyo huduma yake haiku mchangani ila juu ya msingi. Yeye huchimba mawe yaliyo hai ambayo yanaokoka, na kuyaleta kanisani. Kuta za kanisa zinaitwa kuta za wokovu. Muinjilisti anahubiri wokovu na nafsi zinaokoka, kisha zinatumiwa kujenga kuta za hekalu.

MCHUNGAJI
Mchungaji anayachukua yale mawe na kuanza kuyachionga na kuyatengeneza kwa kuyaunganisha pamoja. Huduma ya kwanza muhimu ya mchungaji ni kutunza waamini wachanga, kwa kuweka misingi wa imani. Huduma ya msingi ya mchungaji ni kuchunga na kulisha kundi. Anafanya kazi ya urejesho. **Zab.23:1** ***"Bwana ni mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu."*** Mchungaji anawapa waamini wachanga Neno la Mungu na upendo wa Mungu. Aya **.2** ***"Yeye hunilaza chini kwenye majani mabichi; na katika maji matulivu huniongoza."*** Mchungaji analisha kondoo wachanga chakula kinachofaa, anawapa makaazi ya usalama ambapo wanaanza kukuwa na kutunzwa. Nafsi zao zinarejeshwa.

(Yoh.21:15-17) & (1PET.5:1-2)

MWALIMU
Mwalimu anawachukuwa hawa Wakristo wachanga ambao wametunzwa na mchungaji na kuwaweka kwenye msingi wa Neno la Mungu. Anaanza kuwafanya kuwa wanafunzi. Huduma ya mwalimu ni kufunza Neno ***'kanuni juu ya kanuni, msitari juu ya msitari,'*** (**Is.28:10**). Mwalimu analisha Neno watu ambao wametunzwa ili kwamba huyu mwanafunzi

mchanga akuwe na kuanza kula chakula kigumu, huku akiwahimiza kuendelea mbele na kuufikia utimilifu wanapowekwa kwenye msingi wa Neno. Kisha watakuwa wako tayari kumpokea mtume kuja na kuwaonyesha jinsi ya kufanyika wahudumu. Hawa ambao wamefunzwa watakuwa wako tayari kwa ajili ya utendaji na kukamilishwa kwa kazi. Kizazi kizima cha wahudumu chaweza kukuswa, kizazi kipya cha mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu.

TAMATI

Mtume na nabii wanaweka msingi: msingi dhabiti katika Neno la Mungu. Juu ya msingi huo **muinjilisti anatiwa nguvu kwenda ulimwenguni na kuhubiri wokovu na nafsi nyingi zinaokolewa.** Anajua anaweza kuwarejesha kwa kanisa lililo dhabiti, lenye msingi imara, ambako kuna kikundi cha **wachungaji na wazee watakaotunza hawa wakristo wachanga kwa kuwapa 'maziwa ya Neno'**. Halafu **mwalimu anakuja na kuanza kuwaweka kwa msingi wa Neno la Mungu, akiwafundisha** katika kuwaweka kwa msimgi. Kisha wanaendelea kufunzwa na kujengwa nao waanze kuwafundisha wengine, kuendelea katika upako na kuwahudumia wengine nguvu za Mungu.

SURA YA 1

HUDUMA KATIKA UTANO KATIKA CHUO CHA MATENDO YA MITUME

MUNGU ANAJENGA NYUMBA YA UTUKUFU

Efe.2:19-22 Watakatifu ni wenyeji wa nyumbani mwake Mungu, wamejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii. Msingi ni sehemu ya nyumba ambayo iko chini ya arthi, haionekani. Nyumba bila msingi mzuri itaanguka. Yesu Kristo Mwenyewe ni **Jiwe kuu la pembeni**, **ndiye anayeungamanisha vitu vyote pamoja, ambaye kuta hujengwa juu yake!** Yeye ndiye anayeidhinisha mitume na manabii kuhudumu. Muinjilisti, mchungaji na mwalimu huduma yao iko juu ya ule msingi. Yesu pia ni lile jiwe la kuweka juu kabisa la huo mjengo, yaani, ndiye anayeunganisha vitu vyote mahali pake. (linganisha na **Zak.4:7**)

Chuo cha **Hagai** [ambaye alikuwa nabii wa urejesho baada ya uhamisho wa Yuda kule Babeli] ananena juu ya **utukufu wa nyumba ya mwisho kuwa mkuu kuliko nyumba ya kwanza** (**Hag.2:9**). Hekalu la mwisho linaenda kujazwa na utukufu Wake. Tafsiri ya unabii waeleza kwamba **nyumba ya kwanza ni kanisa katika Chuo cha Matendo ya Mitume**. Mungu anajenga nyumba itakayosimama katika siku hizi za mwisho. Kanisa hili la nyakati za mwisho, nyumba ya Bwana, litakuwa tukufu sana kuliko lile la Matendo ya Mitume. Yote yaliyodhihirishwa katika Chuo cha Matendo kuhusiana na karama na huduma inaenda kurejeshwa. Hakuna ufunuo nje ya Neno ola Mungu; ila **urejesho wa kile kinachonenwa katika Neno la Mungu** (**Matendo 3:19-21**).

Tunajifunza kutoka kwa Kitabu cha Matendo ya Mitume kuona jinsi ya kuanza na kuendelezwa kwa huduma ya Karama tano katika kanisa la kwanza na kufahamu urejesho wa huduma hizo katika kanisa la leo.

MITUME KUMI NA WAWILI WA MWANA KONDOO

Matendo1:16-26 kujaza pengo la Yuda Iskariote. kulikuwa na **Mitume kumi na wawili wa Mwana Kondoo**; Yuda alikuwa msaliti na kwa hivyo ilifaa nafasi yake kujazwa.
Matendo1:21-22 inaelezea mambo muhimu ya kuzingatiwa ili mmoja awe Mtume wa Mwana Kondoo. **Yule ambaye alifwatana na Yesu tangu ubatizo wa Yohana, hata siku ile alipochukuliwa na kwenda juu, na awe shahidi wa wa kufufuka kwake.** Ni watu wawili tu ndio waliohitimu bali Mathiya alichaguliwa. Hawa tu ndio mitume wa Mwana Kondoo (**Ufu.21:14)**. Mitume wengine wanaotajwa katika Kitabu cha Matendo ni wale mitume wa huduma baada ya Yesu kupaa.

> ***Mitume kumi na wawili wake Mwana Kondoo ndio walioanzisha kanisa la kwanza, Walichaguliwa na Bwana wakati wa huduma yake ya kwanza hapa duniani na majina ya hawa kumi na wawili ni misingi ya ukuta wa Mji Mtakatifu (Ufu.21:14).***
>
> ***Mitume wengine wamechaguliwa na Roho Mtakatifut (Mate.13:2-3 & 1Kor.12:28) na kupokea karama ya huduma ya utume (Efe.4:7-12).***

Matendo 2:14 mitume walifanya kazi kama **kikundi** [Yesu alikuwa amewafundisha kufanya kazi pamoja]. Petro alisimama pamoja na wale thenashara na kunena kwa niaba yao.
Matendo2:42 walifundisha **Fundisho la mitume nyumba kwa nyumba;** mitume walienda katika mikutano ya nyumba wakifundisha mafundisho ya Yesu.
Matendo 6:4 Mitume walitangaza lengo la huduma ya Utume: ***"sala na huduma ya Neno"***.

FILIPO MUINJILISTI

Matendo 7 inanukuu mateso na kifo chake Stefano, **wa kwanza kuaua kwa ajili ya imani yake**.

Matendo 8:1 Matokeo baada ya kuaua kwake Stefano kulileta mateso juu ya kanisa na wakristo wa Kiyahudi kutawanyika. *"Walienda kila mahali wakihubiri Neno"* (**a.4**) Walikuwa **watu wa kiutume!** Kwa hivyo, kanisa lilienea kutoka Yerusalemu hata Yudea na Samaria.

Matendo 8:4-8 Filipo alienda kuhubiri Samaria; alikuwa **muinjilisti**. Pia alikuwa akitenda miujiza. Watu waliponywa na kukombolewa alipokuwa akihudumu. Katika **Matendo 21:8** Filipo anaitwa Muinjilisti, lakini huduma yake ilianza kufanya kazi hapa Samaria. Alienda kote akimuhubiri Kristo, kwa ishara nyingi na maajabu na wengi wakaokoka.

Matendo 8:14 Mitume wapokea ujumbe kuhusu yale yaliyokuwa yakiendelea kule Samaria na wakawatuma Petro na Yohana. Wakristo wachanga walikuwa bado hawajapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

Matendo 8:17 Mitume wakawawekea mikono juu yao kisha wakapokea Rohop Mtakatifu.

Mitume waliwaombea na wakapokea Roho Mtakatifu. Mitume walishuka wakawaendea na kanisa likazaliwa. Muinjilisti hajaitwa kujenga kanisa bali avune nafsi zilizopotea.

Matendo8:26 Filipo aliitwa na Bwana aondoke kwenye uvuvio aende na kumhubiria mtu mmoja.

Matendo8:36-38 Filipo muinjilisti alimwongoza Yule towashi kwa Bwana na kumbatiza [kumbuka

Mk.16:15-16]

Matendo8:40 Filipo tena aliendelea, akihubiri katika miji yote aliyoiendea. Alikuwa na ratiba ya huduma kama muinjilisti.

Matendo21:8 Filipo anajulikana kama muinjilisti.

MJUMBE WA KIUTUME **[linganisha na Tito katika Tito1:5]**

Matendo 11:22 Barnaba alitumwa kutoka Yerusalemu.

Matendo 11:24 Alikuwa mtu aliyejawa na Roho Mtakatifu na Imani. Alienda na kumtafuta Sauli na kumleta Antiokia. Barnaba ni **Mjumbe wa kiutume**: anatumwa kama mumishonari na mitume lakini bado hajawa mtume.

MANABII

Matendo 11:27 Manabii walishuka kutoka Yerusalemu hadi Antiokia.

Huduma ya Unabii ilikuwa tayari inafahamika katika kanisa wakati huu: walitoka katika kanisa la Yerusalemu hadi kanisa la Antiokia. Walipokewa na kanisa la Antiokia.

Matendo 11:28 Agaba nabii alikuwa na maono; alionyeshwa ***'kwa Roho'***, yale yatakayo tukia. Yale aliyotabiri yalitimia. [Hii ni ishara ya nabii wa kweli, **Kumb.18:21-22**].

WAZEE: JE, NI WACHUNGAJI?

Katika **Matendo11:30 wazee** wanatajwa mara ya kwanza. Huduma yao ni gani?

Karama zote za huduma zaweza kufanya kazi kama wazee, jinsi Petro anavyosema kuwa yeye ni mzee, japo pia ni mtume (**1 Pet.5:1**). Hata hivyo, uchunguzi unaweza kufanywa katika maandiko matakatifu kwamba **wazee has asana ni wachungaji**, waangalizi, na wachungaji wa kundi la Mungu.

Matendo20:28, ***"jitunzeni … kwa kundi lote, ambamoRoho Mtakatifu amewafanya waangalizi, kuchunga kanisa la Mungu."***

Paulo alikuwa akizungumza na wazee kutoka Efeso.

1Pet.5:2 ***"Kuchunga*** [***kulisha***] ***kundi la Mungu ambalo liko miongoni mwenu, mkihudumu kama waangalizi"***. Petro anazungumza na wazee!

Kwa hivyo ni wazi kwamba wazee ni wachungaji. Paulo pamoja na Petro kwa uwazi walinena juu ya Wachungaji.

WAALIMU

Matendo 13:1 Waalimu wanatajwa pamoja na manabii katika kanisa la Antiokia.
Hii ni mara ya kwanza kutajwa kwa karama ya **mwalimu**; huduma ya uongozi wa kanisa, pamoja na manabii. Inaonekana wazi kwamba waze walijumuisha manabii na waalimu kule Antiokia.

KARAMA YA LIYEPAA YA MTUME

Katika **Matendo 13**, Paulo na Barnaba wanatawazwa na kisha kutumwa kama mitume. Hakika hawa wawili sio miongoni mwa wale kumi na wawili wa Mwana Kondoo; ni watu wa kwanza kupokea karama ya huduma ya Aliyepaa ya utume, baada ya wale wa asili kumi na wawili.
Matendo 13:2 Roho Mtakatifu aliwanenea na kuwambia wawawekee mikono Sauli na Barnaba na kuwatuma kama **mitume**. Manabii na waalimu walichukuwa wakati katika maombi na kufunga, wakimhudumia BWANA, kasha **Roho Mtakatifu akawanenea.**
2 Tim. 1:11 Paulo alijitambua kama **mhubiri [muinjilisti], mtume na mwalimu**.
(kila huduma tano zahitaji msingi imara wa Neno la Mungu; mafundisho yaliyo hai ndicho kigezocha kwanza).

Matendo 14:4&14 Paulo na Barnaba wanajulikana kama mitume. Walikuwa wametumwa na manabii na waalimu, napia wametumwa nje na Roho Mtakatifu.
Paulo na Barnaba **wametawazwa kuwa mitume kulingana na Neno lake Roho Mtakatifu**. **Walipokea karama ya huduma yake Aliyepaa ya utume** (**Efe.4:11**)

MITUME na WAZEE

Matendo 15:6 Kanisa ya Yerusalemu sasa lina mitumena wazee wanaokusanyika pamoja kushughulikia jambo. Bado haijakuwa wazi kutoka kwa Maandiko Matakatifu kama wazee ni huduma yake yeye aliye paa, lakini ni wazi kwamba wanawajibu wa maongozi katika kanisa. Tayari tumenena kuwa wazee hakika ni wachungaji, ama kama wanahusika na na karama nyingine ya huduma. Wazee waliohudumu katika kanisa la Antiokia walikuwa manabii na waalimu (**Matendo 13:1-4**).
Matendo 15:22 Yuda na Sila waliteuliwa kama *"viongozi kati ya watu";*
Matendo 15:32 *"wao wenyewe wakiwa manabii";* walikuwa miongoni mwa ***"mitume na wazee"*** waliokusanyika kwa ajili ya mkutano wa baraza; ni wazi kwamba **walikuwa wazee** pia manabii.
Matendo 15:13 Yakobo, ndugu wa Yesu, pia ni **mzee kiongozi katika kanisa hili**. Kama mtume (**Gal.1:19**), **ananena na mamlaka kuhusu swala la imani na matendo**. Yakobo ana neno la kupambanua hukumu. Pengine katika hali hii, Yakobo akiwa anatumika kama mchungaji 'mkuu'katika kanisa lao la nyumbani Yerusalemu. **Yakobo ananena kwa mamlaka kama mtume** katika maswala ya imani [akitafsiri maandiko matakatifu] na matendo.

KATIKA KITABU CHA MATENDO, TUNAONA MITUME WAZI WAZI, MANABII, WAALIMU, MUINJILISTI NA WACHUNGAJI [yaani baadhi ya wazee].
HUDUMA TANO ZINAFANYA KAZI

MANABII WANATUMWA NA MITUME

Matendo 15:27 mitume na manabii "Yudas na Sila", pamoja na Paulo na Barnaba.
a.32 *"Judas and Silas, themselves being* ***prophets***, ***exhorted and strengthened the brethren with many words****".*

Matendo 15:36 Paulo anaamua **kutembelea tena kila mji** ambao awali alikuwa ame wahubiri injili.
a.37-39 kulikuwa na hali ya kutoelewana kati yake Paulona Barnaba kuhusu kusika kwake Marko.
a.40 Paulo anaamua kuenda na Sila, nabii, pamoja naye.
Mtume na nabii wanajiunga pamoja kuhudumia makanisa.

KIKUNDI CHA MITUME

TIMOTHEO ANAJIUNGA

Matendo 16:1-3 Paulo anaamua kumchukua kijana Timotheo kwenye kikundi; ***"alinenewa vema na wandugu"***. Kikundi cha mitume kinaendelea kukua!
v.5 Uinjilisti unaendelea kutendeka wakati mitume na manabii wanaporudi na kuwatia nguvu.
Kanisa lilikuwa likiongezeka watu kila siku.

UONGOZI WA ROHO MTAKATIFU

Matendo 16:6-7 Kikundi cha mitume kinaongozwa na Roho Mtakatifu.
v.9-10 Paulo anayatii ***"maono"*** aliyopokea na kisha anajipanga kusafiri vilivyo.

KUTOKA KWA MKUTANO WA MAOMBI HADI KWA KANISA LA NYUMBANI

Matendo 16:15 kanisa katika mji wa filipi lilichipuka kutokana na **mkutano wa maombi** (a.13) na likaanzishwa **nyumbani,** na Paulo mtume na kikundi chake.

HUDUMA YA KIKUNDI

Matendo 20:4 Paulo, mtume, aliambatana na kikundi alipokuwa akisafiri.

PAULO AKIWA KORINTHO ALIFUNDISHA

Matendo 18:3 Mtume Paulo alijiandaa kutenda kazi ya mikono yake wakati mwingine.
a.4 Paulo aliingia katika sinagogi kwanza lakini mara nyingi alikataliwa, japo wengine walimwamini.
a.7 Paulo alijiondoa katika sinagogi na kuhudumu katika **nyumba za marafiki** – ***"wakorintho wengi, wakasikia, wakaamini na wakabatizwa"***.
a.11 ***"Na akaendelea mahali hapo mwaka mzima na miezi sita, akifundisha Neno la Mungu miongoni mwao"***. Paulo alitumika kama **mwalimu**.

KITUO CHA MAFUNZO CHA MITUME

Kule Efeso, mtume Paulo aliliweka kanisa juu ya msingi uliohakika; kisha akaanzisha kituo cha mafunzo ambacho kupitia hapo uvuvio ulienea katika mkoa wote wa Asia.
Matendo 19:1-7 Kuweka **misingi** (**Ebr.6:1-2**) ya kanisa la Yesu Kristo.
a.9-10 Kuanzisha **kituo cha mafunzo**; **kufunza kila siku** katika kituo hiki; matokeo yakawa ***"wote waliokaa Asia walisikia Neno la Bwana Yesu, Wayahudi kwa Wayunani"***.
a.11 ***"Na Mungu akafanya miujiza isiyokuwa ya kawaida kwa mikono ya Paulo".***
a.12-17 pepo walitoka;
a.19 wengi ***"wale waliotumia mambo ya uganga wakakusanya vitabu vyao, wakavichoma moto mbele ya watu wote"***.
a.20 *"Kwa hivyo* ***neno la Bwana lilizidi na kushinda kwa nguvu."***

Wote waliokaa Asia walisikia Neno! Hapa kuna **mfano wa huduma ya mitume** ambayo tunastahili kuiga! Paulo hakuondoka mjini bali alifunza kila siku katika shule ya Tirano. Wahubiri [wainjilisti] na wahudumu wengine waliondoka katika kituo hichi cha mafunzo ya mitume na kufanya kazi ya huduma.

ISHARA ZINGINE ZA MTUME

Matendo 20:7&11 Paulo wakati mwingine alinena kwa urefu! Kama mtume, Paulo alifunza na kushuhudia kwa urefu, akihimiza makanisa kila wakati alipoona fursa katika Neno la Mungu.
a.8-10 Eutiko anafufuliwa! Ishara kuu na maajabu yaliambatana na mitume. (**Matendo 2:43**)
Matendo 28:3-6 ***"watashika nyoka"*** (**Mk.16:18**); Paulo hakudhurika nyoka aliponing'inia juu ya mkono wake!
a.7-8 ***"Paulo aliwekea mikono yake juu yake na akamponya"; "watawawekea wagonjwa mikono nao watapata kupona"***, **Marko 16:18.**

KUFWATILIA, KUTUNZA MAKANISA

Matendo 20:17: Paulo alituma wazee wa kanisa la Efeso kuitwa; alikuwa amewateua wazee huko.
a.20: Paulo alikuwa na shule ya mafunzo mchana kutwa Efeso na kuhudumu nyumba kwa nyumba kila jioni.
a.27 Mitume wanatakikana **kutangaza *"kusudi lote la Mungu".***
a.28 Paulo akinena na wazee wa kanisa la Efeso. ***"Jitunzeni nafsi zenu na makundi yaliyokwenu ambayo Roho Mtakatifu amewafanya kuwa waangalizi, na wachungaji wa kanisa la Mungu."*** Ananena na wachungaji.

KARAMA KADHAA NA HUDUMA ZINAZOFANYA KAZI KANISANI

Matendo 21:8 Paulo na kikundi wanakaa na Filipo **muinjilisti**.
a.9 Binti wa Filipo ***"walitabiri";*** **karama ya kutabiri**.
a.10 Agaba **nabii** alishuka kutoka Yudea.
a.18 wazee wote pamoja na Yakobo walikuwepo. Yakobo alikuwa mtume, lakini utme wake ni kama kiongozi wa kanisa kubwa la Yerusalemu, na historia inanukuu kwamba Yakobo alikuwa na ushawishi mkuu juu ya dini ya Wayahudi ya nyakati hizo. Aliuawa na viongozi wa kiyahudi kwa ajili ya imani yake.

YESU ALISEMA MITUME WAKE WATAMSHUHUDIA MBELE YA MABARAZA, KWENYE MASINAGOGI, KWA WATAWALA NA WAFALME(**Mt.10:17-20**)
Matendo 22:1-21 Paulo anawashuhudia Wayahudi Yerusalemu.
Matendo 23:1-10 Paulo anashuhudia mbele ya baraza.
Matendo 24:10-21 Paulo anashuhudia mbele ya watawala.
Matendo 26:1-23 Paulo anajitetea mbele ya mfalme. *"Sikuyaasi yale* ***maonoya mbinguni****"*
Matendo 27:23 Paulo **anatembelewa na malaika kutoka kwa Mungu;** wahudumu wa meli watakuwa salama! **Ni mwito na karama ya Mungu!**

MTUME ANAENDELEA KUFUNDISHA NA KUHUBIRI

Matendo 28:30-31 Paulo, "***akihubiri ufalme wa Mungu na kufundisha mambo kuhusu Bwana Yesu Kristo***".

TAMATI

Katika fundisho hili, tumeangalia kwa ufupi kutoka kwa Maandiko Matakatifu jinsi huduma tano zilivyokua katika Kitabu cha **Matendo**, na kuona huduma zote zikifanya kazi.

Sura ya 2

KARAMA YA HUDUMA YA MTUME.

MTUME maana yake ni "aliyetumwa", mjumbe maalum, Yule ambaye ametumwa kutekeleza wajibu Fulani, Yule anayetumwa kwenda na ujumbes. Jambo muhimu kuhusu huduma ya utume ni kwamba Mungu ndiye anayemuita mtume, anamuinua, hasa baada ya miaka mingi ya mafundisho na maandalizi, kisha anamtuma huyo mtu kufanya kazi ya utume.

Mambo matatu muhimu kuhusu mtume:

1. ***'Ni yule ambaye amekutana au kumwona Kristo aliyefufuka.'*** Hii maana yake ni nini? Paulo mtume hakumwona Yesu akiwa katika mwili lakini alikutana na Bwana aliyefufuka akielekea Dameski. Vivyo hivyo, Stefano ambayealiuwawa kwa imani yake pia alimwona Yesu aliyefufuka alipokuwa akipigwa kwa mawe. Ushuhuda wangu ni kwamba mwito wa mtume unatakiwa ujulikane kwa msingi uliowazi wa kukutana au kuonana na BWANA, kwa sababu kuna ubishi mwingi juu ya huduma hii.

2. ***'Ni Yule anayepanda makanisa.'*** Mtume ni mjenzi wa kanisa.

3. ***'Ni Yule anayehudumu kwa ishara maajabu na miujiza.'*** Kila karama ya Yesu aliyefufuka inatarajiwa kutumika kwa ishara na maajabu. Mwito wa utume unatakiwa uthibitishwe na Bwana kwa njia hii, kikamilifu. **Matendo ya Mitume 2:43 *"… ishara nyingi na maajabu zikafanywana na mitume."***
   2Kor.12:12 *"Kweli ishara za mitume zilizotendwa katikati yenu katika saburi yote, kwa ishara na maajabu na miujiza."*

Bwana anawaita watu kwa majina kuwa mitume
Mitume wanatiwa nguvu na Bwana kutoa pepo wachafu na kuponya wagonjwa
Mitume wanatumwa na Bwana kwa makundi Fulani ya watu.

KUITWA KWAO MITUME

Katika **Matt. 10** twasoma juu ya kuitwa kwao mitume wa kwanza na Bwana Yesu Kristo. Mwito wa kwanza sisi sote tunaoupokea ni wa kumfwata Kristo; **kisha uteuzi kwa huduma Fulani**. Miongoni mwa watu wengi waliomfuata Yesu, Mungu aliwaita thenashara kuwa mitume.
Mt.10:1 *"Akawaita wanafunzi wake kumi na wawili akawapa amri juu ya pepo wachafu wote wawatoe na kupoza magonjwa yote na udhaifu wa kial aina."* Ishara za utume zilizotolewa na Yesu ni nguvu juu ya pepo wachafu na uwezo wa kuwaponya wagonjwa.
Katika **Matt. 10:2-4** Yesanawataja wale ambao watakuwa mitume wake. **Aliwaita kwa majina**. Walichaguliwa na Yesu baada ya kukesha usiku kucha akiomba Baba Yake. (**Lu. 6:12–16**)
a.5-6 mitume wanatumwa nje na Bwana. Aliwapa maagizo maalum: ni kwa watu gani walikuwa wawaendee, na kule ambako hawakustali kwenda.
a.7-8 inanena juu ya kile ambacho mitume wanastahili kufanya. Wanatakiwa ***"…kuhubiri, wakisema, 'Ufalme wa mbinguni umekaribia.' Ponya wagonjwa, watakase wakoma, wafufue wafu na kutoa pepo wachafu."***

Mt. 10:9-15 jinsi ya kuendeleza huduma. Walitumwa na Bwana na wakawa watiifu kwa maagizo Yake. Mitume watateswa wakati ambapo watakuwa wakihudumu.

Mitume watateswa kwa mwenendo wa huduma ya kitume
a.16-20 Mateso yatajitokeza wakati watu wanapochukua hatua ya kuondoka kwenda kutekeleza huduma kwa ajili ya Bwana, hata kutoka kwa jamii. Mitume walikuwa watarajie mateso lakini bila kuogopa kwa sababu Roho Mtakatifu atawapa kile watakacho sema (a**.19-20)**.
a.27-31 Mtume anatakiwa **awe tayari kuutoa uhai wake**.
a.32-33 Kisha ameitwa **kumkiri Kristo mbele ya watu**; ukifanya hili, Yesu anaahidi kukiri jina lako mbele ya Baba.
a.34-39 kutakuwa na migawanyiko na fitina. ***'Asiyeutwaa msalaba wake na kunifuata Mimi hanifai'*** (**a.38**).

Anayempokea mtume, ampokea Kristo
Mt. 10:40-42 Kuna dhawabu kwa wao wanaowapokea mitume. Yesu alisema [akiwanenea mitume] ***"Anayewapokea ninyi anipokea Mimi, naye anipokeaye Mimi ampokea Yeye aliye nipeleka Mimi."*** Ukimpokea mtume, unampokea Bwana **(a.40**). bwana hasemi hili kwa mwingine awaye yote!

MITUME KUMI NA WAWILI WA MWANA KONDOO

Mitume walikuwa naya Yesu kwa mda kabla ya kuwataja. Walikuwa tayari wamepokea mafunzo kidogo kutoka kwake Yesu. Aliwajua. **Ufun. 21:14** Katika Yerusalem Mpya, kuta za mji zimejengwa juu ya misingi ya Mitume Kumi na Wawili wa Mwana Kondoo. Kuta hizi zimejengwa kwa mawe yaliyohai, (**1 Pet.2:5**)
Kuna mitume 12 tu, wa Mwana Kondoo. Katika **Matendo 1:15-26** twasoma kuhusu kujaza pengo la Yuda aliyemsaliti; alihitajika awe: **Yule ambaye amekuwa na Yesu tangu kubatizwa Kwake na Yohana hadi kupaa Kwake** (21-22).

Kulihitajika mitume 12 wa Mwana Kondoo.

Kanisa linajeengwa kwa misingi ya mitume. **Efe.2:20, *"Yesu Kristo Mwenyewe akiwa Jiwe Kuu la Pembeni."*** Mitume, wale kumi na wawili pamoja na wale waliopokea huduma yake Yesu aliyepaa, ni wahudumu wa misingi ambaokupitia kwao kanisa la kiutume lake Bwana Yesu linajengwa.

FUNGUO ZA UFALME

Matt.16:18-19. Yesu alimpa mtume Petro funguo za Ufalme.
Petro anatumia funguo:
Yerusalemu - **Matend. 2:17-41** Petro alichaguliwa na Mungu kusimama pamoja na wale kumina mmoja na kuhubiri Siku ya Pentekoste na matokeo yake Wayahudi 3000 wakafunguliwa kuingia katika Ufalme. Mnamo siku hiyo, Petro alitumia funguo kufungua Ufalme wa mbinguni kwa ajili yawale Wayahudi 3000.
Samaria – **Matend. 8:14-17** Baada ya Filipo kuhubiri Samaria kama muinjilisti aliyefaulu kwa ishara na maajabu, wanaume kwa wanawake waliamini na kubatizwa, lakini walikuwa bado hawajapokea Roho mtakatifu. Kanisa la Yerusalemu likawatuma Petro na Yohana, viongozi wawili wa mitume, ambao baada ya kuwawekea mikono walipokea Roho Mtakatifu. Petro aliutimiza utume wake kwa kutumia funguo kwa kufungua ubatizo wa Roho Mtakatifu Samaria.
Kaesarea – **Matendo 10:30-46** Petro alienda kwa nyumba ya Kornelio, Myunani, kuishiriki injili kwa kutumia funguo kumhubiri Yesu, na hata kuwachilia Roho Mtakatifu kwao. Kisha akawabatiza katika maji. Petro aliwafungulia mataifa ufalme wa Mungu.
Petro ametumiwa kama mtume wa msingi katika njia maalum tatu katika Kitabu cha Matendoya Mitume katika kutimiza Tume Kuu (**Matend. 1:8**).

Paulo, mtume, alikuwa na funguo kama hizo za Petro na alizitumia.
Paulo alipokea funguo hizo mara ya kwanza wakati ule Anania alipotumwa kwake kumponya, ajazwe na roho Mtakatifu na kubatizwa katika maji. **Matendo 9:15-16** twasoma kuhusu utume wa Paulo aliopewa na Yesu kupitia kwake Anania, ***"yeye ni chombo change kiteule alichukue jina langu mbele ya mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli".*** Wakati Anania alipomwekea mikono, aliachilia nguvu za hizo funguo za Ufalme wa Mbinguni.
Katika **Matendo 13:1-4** Paulo anatumwa kama mtume na Roho Mtakatifu kufanya kazi ya huduma utume. Kabla ya hayo aliitwa mwalimu. Tayari anatambulika kuwa na kazi ya huduma ya uwalimu. Kanisa lilikutana pamoja ***'likamhudumia Bwana na kufunga,'*** halafu Roho Mtakatifu akanena kwao ***"Sasa nitengeeni Barnaba na Sauli kwa ajili ya kazi ambayo nimewaita kufanya".*** Manabii wale wengine na waalimu wakawawekea mikono na kuwaachilia waende.
Katika **Matendo 14:1-4** Paulo na Barnaba wanaanza kuhudumu kama mitume, wakihubiri na kufundisha Wayahudi na Wayunani, wakiwaleta wengi kwaBwana huku kukiwa na upinzani mwingi. Katika aya ya 3 tunasoma kwamba Bwana ***"Bwana aliyelishuhudia neon la neema Yake, akiwajaalia ishara na maajabu yatendeke kwa mikonoyao."*** Ishara na maajabu hufwata mitume!

Katika **Matendo 19:1-7** tunaona Paulo akitumia Funguo za Ufalme katika kwa kupanda kanisa Efeso.

Paulo alitumiaje funguo Efeso?
1. **Alimhubiri Yesu kwao.**
2. **Waalibatizwa katika jina la Yesu.**
3. **Walipokea Roho Mtakatifu, wakanena kwa lugha mpya na kutabiri.**

Hawa kumi na wawili ndio mawe ya msingi ya kanisa la Efeso.

MITUME KATIKA CHUO CHA MATENDO YA MITUME

Matendo 2:38 'Petro akawaambia, ***"Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."'***
Hapa tunamwona Petro akitumia funguo: akiwaita watu kutubu, wabatizwe katika Jina lake Yesu Kristo na kupokea Roho Mtakatifu.

Matendo 8:14-15 ***'Na mitume waliokuweko Yerusalemu, waliposikiaya kwamba Samaria imelikubali Neno la Mungu wakawapelekea Petro na Yohana; ambao waliposhuka, wakawaombea, wakampokea Roho mtakatifu.'***

Mtume anatumiwa kumwachilia Roho Mtakatifu.

Matendo 9:15-16 'Lakini Bwana akamwambia, ***"Nenda tu, kwa maana huyu nichombo kiteule kwangu, alichukue jina langu mbele ya mataifa, wafalme na wana wa Israeli. Maana nitamwonyesha yalivyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili ya Jina Langu."***

Paulo mtume aliitwa na kutumwa na Yesu.

Matendo 10:1-44 Petro alitumwa na Bwana kwenda kwa nyumba ya Kornelio, kwa mataifa walioamini. Alimhubiri Yesu kwao, Roho Mtakatifu akawashukia na kuwabatiza walioamini.

Petro mtume anaweka msingi wa kanisa.

Matendo13:4 ***'Wakiisha kupelekwana Roho Mtakatifu…'*** **Ni Roho Mtakatifu ndiye anayemtia mtu mafuta na kumtuma.** Paulo na Barrnaba wanatumwa kwenda kufanya kazi ya huduma ya mitume.

Matendo 14:21-23 ***'Hata walipokwisha kuihubiri Injili katika mji ule, na kupata wanafunzi wengi, wakarejea mpaka Listra na Ikonio na Antiokia, wakifanya imararoho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile imani, nay a kwamba imewapasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi. Na walipokwisha kuwachagulia wazee katika kilakanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakawaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini.'***

Mitume wanapanda makanisa, wanatia nguvu kanisa, wanateua na kuwachagua wazee [wachungaji]. Wana uwezo wa kupambanua na kujua ni nani anayefaa katika uongozi.

Matendo 18:1-8 Paulo anazuru Korintho na tunaona kazi ya utume ikitendeka: **kanisa linazinduliwa, kazi ya uinjilisti inatendeka na Neno la Mungu linafunzwa**. Huu ndio ulikuwa msingi dhabiti wa kanisa lililozinduliwa Korintho lililotembea katika ishara na maajabu.

Matendo 19:1-7 Efeso, misingi inawekwa katika maisha ya watu binafsi na kanisa linapandwa. **Katisa kule Efeso lilikua na kufanyika kanisa hodari la kimitume na uinjilisti huku karama zote za huduma zikifanya kazi.**

HUDUMA YA MTUME

1. Mitume wanaitwa kwa jina na kutumwa na Bwana Kwenda. Marko 3:13-19
a.13, **Yesu alipanda mlimani** *'akawaita aliowataka*.'
a.14-15, *'Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, tena wawe na amri ya kutoa pepo na kuponya wagonjwa'***.**
Matendo 13:1-4 Roho mtakatifu aliwatambua Sauli na Barnaba na kuwatenga ili watumwe.

2. Mitume wanatumika kupanda makanisa na kuweka misingi.
K atika **Matendo 2,** Petro mtume anaweka misingi siku ya Pentekoste alipowaambia,
'Tubuni kila mmoja wenu, na mkabatizwe kwa Jina lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, na mtapokea kipawa cha Roho mtakatifu.'
Katika **Matendo 8** mtume Petro na Yohana wanatumwa kwenda Samaria ambako Filipo alikuwa akihubiri. Wakawaombea wakristo wachanga wakapokea Roro Mtakatifu, **(a**.15**).**
a.17 *'**wakawawekea mikono, wakapokea Roho Mtakatifu***. Misingi inawekwa**.**
Matendo 10 yanukuu Petro akiwa katika nyumba ya Kornelio. Anamhubiri Yesu kwa Mataifa, Roho mtakatifu anawashukia naye Petro anaamuru wabatizwe. Kanisa limepandwa.
Katika **Matendo 19:1-7** mtume Paulo anatumiwa kupanda kanisa Efeso. Wanafunzi wabatizwa katika jina lake Bwana Yesu. Halafu Paulo ***'akawawekea mikono, Roho Mtakatifu akawashukia wakanena kwa lugha mpya na wakatabiri'*** (a.**6**).

3. Mitume wamepewa uwezo na Yesu kuponya, kutakasa, kufufua wafu na kutoa pepo wachafu. Katika **Mathayo** Yesu anawatuma wale kumi na wawili na anawaamurisha katika aya ya **.8** "***poza wagonjwa, takasa wakoma, fufua wafu, toa pepo wachafu."***

Tendo hili linarudiwa katika **Mk.3:15,** ambako Yesu aliwapa uwezo ***"kila magonjwa na kutoa pepo wachafu".*** Hii ni sehemu ya Tume Kuu ambayo Yesu aliwapa Mitume kabla ya kupaa mbinguni, **Mk.16:17-18** ***"Na ishara hizi zitawafwata waaminio, kwa Jina langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; watawashika nyoka; na wakinywa chochote cha kuvifisha, hakitawadhuru; watawawekea mikono wagonjwa nao watapata afya."***

Mitume wanahubiri injili kwa ishara na maajabu: **Rum. 15:18-19,** Paulo anaandikia kanisa lililoko Roma, ***"Maana sitathubutu kutaja neno asilolitenda Kristo kwa kazi yangu, Mataifa wapate kutii, kwa neon au kwa tendo, kwa nguvu za Roho mtakatifu, hata ikawa tangu Yerusalemu, na kando kando yake, mpaka Iliriko, nimekwisha kuihubiri Injiliya Kristo kwa utimilivu.".***
Injili bila nguvu sio Injili kabisa!
2 Kor.12:12 ***"Kweliishara za mitume zilitendwa katikati yenu katika saburi yote, kwa ishara na maajabu na miujiza."***

4. Mitume wanatumiwa kuweka Roho Mtakatifu. Katika Matendo **8** Filipo alishuka Samaria na kuwahuubiri habari za Kristo. Wengi waliitikia, waliamini na wakabatizwa. **Aya 14-17** ***"… Ndipo wakaweka mikono yao juu yao nao wakampokea Roho Mtakatifu."***
Katika **Matendo 10** Petro anawahubiri Mataifa katika nyumba ya Kornelio. **A.44** ***"Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno."***
Katika **Matendo 19** Paulo alishuka Efeso na kukutana na kikundi cha wanafunzi na kuwauliza kama wamempokea Roho Mtakatifu. Wakamjibu, ***'la hasha kusikia kwamba kuna Roho Mtakatifu hatukusikia'*** (a**.2**). Paulo akawafunulia maandiko matakatifu na ***'akaweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao wakaanza kunena kwa lugha na kutabiri'*** (a**.6**)**.**

5. Mitume wana mamlaka kutoka kwake Yesu kufunga na kufungua.
Matt.16:19 ***'Nami nitakupa wewe funguo za ufalme wa mbinguni na lolote utakalo funga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni. Na lolote utakalo lifungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni'***.
Matt.28:18 ***'Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani'.*** **Yesu aliwapa mamlaka Yake mitume Wake,** ***Luka 10:19 'Tazama nawapa mamlaka kukanyaga nyoka na nge na nguvu zote za adui. Na hakuna chochote kitakacho wadhuru.'***

6. Mitume wameitwa kwa huduma ya maombi na neno.
Katika **Matendo 6:1-4** mnong'ono ulizuka kati ya Wayahudi wa kiyunani na Waebrania kwa sababu ya wajane wao waliosahauliwa katika huduma ya kila siku. Mitume waliamua kuchaguliwa kwa wasaidizi saba kushughulikia swala hilo.
a.*2-4 'Wale thenashara wakawaita jamii ya wanafunzi, wakasema haipendezi sisi kuliacha neno la Mungu na kuhudumu mezani. Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; na sis tutadumu katika kusali na kulisimamia lile neno."*

7. Mitume wanaendeleza uongozi wa juu kwa kuwakuza wengine katika kaziya huduma. Matendo **6:1-7** Saba wengine wakachaguliwa katika kusaidia katika utendaji wa kazi; wanachaguliwa kwa kuwekewa mikono. Matokeo ya huduma inayoongezeka: ***"neno la Mungu likaenea, hesabu ya wanafunzi iliongezeka pakubwa."***

8. Huduma ya Mtume inahisisha uchungaji, kulisha na kulinda kundi. Mtume Petro alichaguliwa na Yesu kwa huduma ya uchungaji.
Yn. 21:15-17 Yesu alimwagiza Petro ***"Lisha wana-kondoo wangu", "Chunga kondoo zangu",*** na tena ***"Lisha kondoo zangu".***

9. Mitume wanatakiwa kuhudumu hadharani na nyumba kwa nyumba.
Matendo 2:42-47 kanisa la kwanza lilifundishwa ***'Funzo la mitume'*** na ***'na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu wakimega mkate nyumba kwa nyumba'***.

Katika **Matendo 20:20** Paulo ananena na kanisa la Efeso, akiwakumbusha jinsi alivyowahubiri Injili na ***'kufundisha hadharani na nyumba kwa nyumba'.***

10. Mitume wanastahili kuhubiri habari ya kusudi lote la Mungu.
Paulo kama mtume aliweza kusema kwamba "***hakujiepusha kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu'*** (**Matendo 20:27**)**. Matendo 2:42** inazungumzia juu ya fundisho la mitume ambalo lilifundishwa kanisa la kwanza. **Waebrania 6:1-2** misingi sita imenukuliwa ambayo haina budi kuwekwa kwanza kabla ya kanisa kuendelea na kuufikia utimilifu. Misingi hiyo ni: Kuzitubia kazi zisizo na uhai, kuwa na imani kwa Mungu, mafundisho ya mabatizo, kuwekea mikono, kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele. Mtume anaita kanisa lirudi katika misingi, kuhakikisha ya kwamba imewekwa vizuri. Misingi isipowekwa vizuri, Mungu hataweza kufunua kwa undani neno Lake kwa waaminio.
Yakobo mtume anatangaza kusudi la Mungu kwa baraza lililokuwa Yerusalemu. **Matendo 15:6** ***'mitume na wazee walikutanika pamoja kushughulikia hilo jambo',*** halafu katika **a.13-21** ananena hekima ya Mungu katika hoja hiyo.

11. Mitume wanawachagua wazee.
Mitume walitembelea makanisa katika miji mbali mbali: **Matendo 14:21** ***'na walipokwisha kuwachagulia wazee katika kila kanisa, na kuomba pamoja na kufunga, wakwaweka katika mikono ya Bwana waliyemwamini' (aya ya 23).***
Paulo alimtuma Tito kuwachagua wazee, Tito 1:5 'Kwa sababu hii nilikuacha Krete uyatangeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru'.

12. Mitume wameitwa kuwa na subira na kutaraji mateso na dhiki.
Matt.10:5-15 inaorodhesha maagizo ambayo Yesu aliwapa wale thenashara kabla ya kuwatuma, halafu katika **a.16-26,** Yesu anawaonya kwamba mateso yatakuja. **2 Kor.11:23-28** Paulo anaorodhesha mateso aliyoyapitia kama mtume. Yesu anaonya katika **Lu. 21:16** ***'Nanyi mtasalitiwa na wazazi wenu na ndugu zenu, na jamaa zenu, na rafiki zenu, nao watawafisha baadhi yenu'.*** Maonyo haya yanarudiwa katika **Mk.13:9-13**. Yesu aliteswa na kukataliwa. Aliwaambia wanafunzi wake, ***'Mtumwa sio mkubwa kuliko bwana wake, ikiwa waliniudhi mimi, watawaudhi ninyi.'*** (**Jn.15:20**)**.** Mitume katika kanisa la kwanza waliudhiwa, **Matendo 4:1-22.** Petro na Yohana walitiwa mbaroni na kufungiwa jela, na wakaamurishwa wasihubiri tena katika Jina la Yesu. Paulo alitarajia kuudhiwa kisha akatamatisha hivi katika **1 Kor.4:9** ***'Maana nadhani ya kwamba Mungu ametutoa sisi mitume sisi mitume mwisho, kama watu waliohukumiwa wauwawe; kwa maana tumekuwa tamasha kwa dunia; kwa malaika na wanadamu'.***

13. Mitume wabeba mzigo wa maangalizi ya makanisa yote.
2 Kor.11:27-28 ***"Katika taabu na masumbufu; katika kukesha mara nyingi; katika njaa na kiu; katika kufunga mara nyingi; katika baridi na kuwa uchi."*** Mtume ni kama mzazi anayewachunga watoto wao. Kupitia kwa nyaraka zake, ni wazi kwamba Paulo alikuwa na mzigo wa maangalizi kwa ajili ya makanisa aliyoyatembelea. **2 Kor.12:14** ***'Tazama, hii mara ya tatu ya mimi kuwa tayari kuja kwenu, wala sitawalemea. Maana sivitafuti vitu vyenu, bali nawatafuta ninyi; maana haipasi watoto kuweka akiba kwa wazazi, bali wazazi kwa watoto'.***

14. Mtume yuko tayari kutapanya na kutapanywa kwa ajili ya watakatifu katika makanisa.
Mtume Paulo anawaambia Wakorintho katika **2 Kor.12:15,** ***'Nami kwa furaha nyingi nitatapanya, tena nitatapanywa kwa ajili ya roho zenu. Je! Kadiri nizidivyo kuwapenda sana ninapungukiwa kupendwa?',***

15.Mtume anafanya yote kwa ajili ya kuwajenga wote walio makanisani.
2 Kor.12:19, ***'Mwadhani hata sasa ya kuwa najidhuru kwenu! Mbele za Mungu twanena katika Kristo. Na hayo yote, wapenzi, ni kwa ajili ya kuwajenga ninyi.'***

16. Kristo anajidhihirisha kwa njia kubwa katika huduma ya Mtume.
2 Kor.13:3, ***'kwa kuwa mnatafutadalili ya Kristo, asemaye ndani yangu, ambaye si dhaifu kwenu, bali ana uweza ndani yangu'.***

17. Mtume anaishi na kuhudumu kwa nguvu za Mungu.
Paulo alijua kwamba ni lazima ategemee nguvu za Roho Mtakatifu. **1 Kor.2:1-5,** ***'Lakini nafsini mwangu nilikusudia hivi, nisije kwenu tena kwa huzuni. Maana mimi nikiwatia huzuni, basi ni nani nifurahishaye mimi ila yeye ahuzunishwaye nami? Nami naliwaandikia neno lilo hilo, ili nijapo nisitiwe huzuni na wale ambao nilipasa kuwafurahia; nikiwatumaini ninyi nyote kwamba kwa furaha yangu ni yenu ninyi nyote. Maana kwa dhiki nyingi na taabu ya moyo niliwaandikia na machozi mengi; si kwamba mhuzunishwe, bali mpate kujua upendo wangu nilio nao kwenu jinsi ulivyo mwingi. Lakini iwapo mtu amehuzunisha mimi tu, bali kwa sehemu (nisije nikawalemea mno), amewahuzunisha ninyi nyote.'*** Paulo alitegemea nguvu za Mungu zilizokuwa ndani yake,
2 Kor.13:4, ***'Maana alisulubiwa katika udhaifu, lakini anaishi kwa nguvu za Mungu. Maana sisi nasi tu dhaifu katika yeye; lakini tutaishi pamoja naye kwa uweza wa Mungu ulio kwenu.'***

18. Mtume anajua neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu, **2 Kor.13:14.**

19. Mtume anajua silaha za vita na anaweza kuzitumia vizuri.
2 Kor.10:3-6, ***'Maana ingawa tunaenda katika mwili, hatufanyi vita kwa jinsi ya mwili. Maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uweza katika Mungu hata kuangusha ngome, tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kichiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na kukiteka nyara kila fikra ipate kumtii Kristo; tena tukiwa tayari kupatiliza maasi yote, kutii kwenu kutakapotimia.'***
Mtume anaweza kupatiliza maasi yote.

20. Mitume hawajipimi ama kujilinganisha na wengine. **2 Kor.10:12,** ***'kwa kuwa hatudhubutu kujihesabu pamoja na baadhi yao wanaojisifu wenyewe, wala kujilinganisha nao; bali wao wenyewe wakijipima nafsi zao, na wakijilinganisha nafsi zao, hawana akili.'***

21. Mitume wanajua eneo la huduma ambalo Mungu amewapa.
2 Kor.10:13, ***'Lakini sisi hatujisifu zaidi ya kadri yetu; bali kwa kadiri ya kipimo tulicho pimiwa na Mungu, yaani, kadiri ya kufika hata kwenu.'***

22. Mtume anahubiri Injili akielekea nchi zilizo mbele ya nchi yake.
2 Kor.10:14-16, Paulo anajua kwamba ameitwa ***'kuihubiri Injili katika nchi zilizo mbele kupita nchi zenu, tusijisifu kwa kipimo cha mtu mwingine kwa mambo yaliyokwisha kutengenezwa.'***
Mtume anapaswa kutii amri ya Yesu aliyoitoa katika **Matt. 28:19-20,** ***'Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwishowa dahari.'***

23. Mtume anaweza kutumiwa kuwatambua mitume waongo.
Paulo aliweza kupambanua katika **2 Kor.11:13,** ***'Maana mitume kama hao ni mitume wa uongo, watendao kazi kwa hila, wanaojigeuza wawe mfano wa mitume wa Kristo.'***

24. Mtume anazaidiwa kifedha na baadhi ya makanisa.
2 Kor.11:7-9, mtume Paulo anaelezea kwamba alipokea msaada wa fedha kutoka kwa makanisa mengine ili aweze kuhubiri Injili ***'bila malipo'*** kwa kanisa la Korintho. Mitume wana haki ya kusaidiwa kifedha. **1Kor.9:1-18,** Paulo anawafafanulia Wakorintho kwamba wanaoihubiri Injili wanastahili kusaidiwa ama kulipwa kama yeyote mwingine anye fanya kazi nyingine yeyote.
a13&14 ***'Hamjui ya kuwa wale wazifanyaokazi za hekaluni hula katika vitu vya hekaluni, na wale waihudumiao madhabahu hula katika vitu vya madhabahu? Na Bwana vivyo hivyoameamuru kwamba wale waihubirio Injili, wapate riziki kwa hiyo Injili'.***

25. Mitume wameitwa pia kwa huduma ya kufundisha.
Katika Tume Kuu aliyoitoa Yesu, (**Matt.28:20**) mitume wameamurishwa ***'kuwafundisha mambo yote niliyowaamuru ninyi.'***
Mitume walifundisha ***'fundisho la mitume'*** **Matendo 2:42.** Mtume Paulo alifundisha Wakorintho: **Matendo 18:11**, ***'Akakaa huko kwa muda wa mwaka mmoja na miezi sita akifundisha kati yao neno la Mungu.*** Efeso: **Matendo 19:9-10,** Paulo ***'…akihojiana na watu kila siku katika darasa ya mtu mmoja, jina lake Tirano. Mabo haya yakaendelea kwa muda wa miaka miwili, hata wote waliokaa Asia wakalisikia neno la Bwana, Wayahudi kwa Wayunani'.*** Roma: **Mate. 28:30-31,** ***'Akakaa kwa muda wa mika miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote waliokuwa wakimwendea, akihubiri habari za ufalme wa Mungu na kuyafundisha mabo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu.'***
Paulo alimfundisha Timotheo na kumuagiza kuwafundisha wengine, **2 Tim.2:2,** ***'Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.'***

26. Mitume wakati mwingine wanaachwa upweke.
2 Tim. 4:9-16. Paulo alijikuta kuwa ameachwa, wengine walitaka kudhuru na wengine walimpinga.

27. Bwana ndiye Anayewashikilia mitume.
2 Tim.4:17-18, ***'Lakini Bwana alisimama pamoja nami akanitia nguvu, ili kwa kazi yangu ule ujumbe utangazwe kwa utimilifu, hata wasikie Mataifa yote; nami nikaokolewe kwa kinywa cha samba. Bwana atanikoa na kila neno baya, na kunihifadhi hata nifike ufalme wake wa mbinguni. Utukufu una Yeye milele na milele. Amina.'***

28. Mitume wanastahili kuutesa na kuutumikisha mwili.
1 Kor.9:27, ***'Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.'***

29. Mtume anastahili kuwa na wakujizuia katika mambo yote.
1 Kor.9:25, ***'Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika.'***
Wanastahili kuwa na nidhamu**. Efe.5:18,** ***'Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe na Roho.'***

MAMBO MENGINE SABA KUHUSU MTUME.

1. Mungu amempa mtume uweza wa Maongozi.

Filipi. 3:17 ***'Ndugu zangu, mnifuate mimi, mkawatazame wao waendao kwa kuufuata mfano tuliowapa ninyi'.*** Paulo anasema ***'fuata mfano wangu'***. Mtume anatakikana kuishi maisha yanayoweza kuigwa ama awe kielelezo kwa wengine. ***'Nifuateni mimi jinsi mimi nimfuatavyo Kristo.'***

2. Mtume anaenenda katika mamlaka.

2Pet.3:2 ***'…mpate kuyakumbuka yale maneno yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu, na ile amri ya Bwana na Mwokozi iliyoletwa na mitume wenu.'***

Petro maagizo maalum na Bwana, lakini mamlaka hayo yametolewa na Bwana kwa mitume wote. Watu wa Mungu wanastahili kuchunga maneno yanayoletwa kwao kwa njia ya mitume ambao Mungu anatuma kwao.

3. Maisha ya mtume yanatakiwa kuonyesha Neema.

Rom. 1:5 ***'Ambaye kwa Yeye tulipokea neema na utume ili mataifa yote wapate kujitiisha kwa imni, kwa ajili ya jina lake.'*** Tunapokea neema kwa njia ya Yesu Kristo.

Rom. 12:6 ***'Basi kwa kuwa tuna karama mbali mbali; kwa kadiri ya neema tulivyopewa tuitumie.'*** Kila mmoja wetu amepokea neema lakini kuna neema ambayo mtume anaenenda na kuhudumu katika Mwili. Maisha ya mtume yawe kielelezo kwa ajili ya neema aliyoipokea.

4. Huduma kamilifu ya Mtume.

I Thess.5:23 ***'Mungu wa amani mwenyewe awatakase kabisa; nanyi nafsi zenu na roho zenu na miili yenu mhifadhiwe mwe kamili, bila lawama, wakati wa kuja kwake Bwana wetu yesu Kristo.'*** Mungu yuko anawaleta watakatifu katika utimilifu huu kwa kurejesha huduma tano kwa kanisa. Kuna ukamilifu kwa huduma mtume kwa ajili ya kuleta sura kamili na kulileta kanisa katika utimilifu.

5. Mtume anastahili kuenenda katika ustahi wa uwakili.

Matendo 2:42 ***'Nao walidumu katika fundisho la mitume…'.*** Jinsi torati ya Musa ilivyotawala maisha ya kanisa la kwanza katika Agano la Kale, fundisho la mitume ndilo lililotawala maisha katika kanisa la Agano Jipya.

1 Thess.2:4 ***'Basi kama tulivyopata kibali kwa Mungu tuweke amana Injili, ndivyo tunenavyo; sio kama wapendezao wanadamu baliwampendezao Mungu anayetupima mioyo yetu'.*** Mitume wameaminiwa na shauri lote la Mungu.

6. Uweza wa utawala

2 Kor.11:28 ***'…kando na mambo mengine, yako yanijiayo kila siku, ndiyo maangalizi ya makanisa yote.'*** Paulo ana utawala wa uangalizi kwa makanisa**. Matendo 4:35** ***'…wakaiweka miguuni pa mitume; kila mtu akagawiwa kwa kadiri ya alivyohitaji.'*** Kanisa la kwanza ***'lilikuwa na vitu vyote shirika'.*** Walipotaka kutoa amana ya vitu vyote, walileta miguuni pa mitume na kuomba shauri na dhibitisho la viongozi jinsi ya mgao wa vile vipawa**.**

1 Kor.16:1 ***'Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia nanyi fanyeni vivyo.'***

Tito 1:5 ***'Kwa sababu hii nalikuacha Krete, ili uyatengeneze yaliyopunguka, na kuweka wazee katika kila mji kama vile nilivyokuamuru.'***

2 Tim.4:10-12, Paulo anatumia uangalizi wake katika kutoa maelezo kwa watakatifu.

7. Ubora wa kuziunganisha huduma.

Huduma ya utume ambayo imekomaa inadhihirisha mwenendo wa huduma zingine katika njia zote. **Efe.4:11** ***'Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu.'***

Paulo alidhihirisha ule muungano wa hizo huduma tano. **2Tim.2:7 *'…nami kwa ajili ya huo naliwekwa niwe mhubiri na mtume – nasema ukweli, sisemi uongo, mwalimu wa mataifa katika imani na kweli.'*** Paulo alihubiri Injili kama muinjilisti, alifunza Neno na kuhudumu kama mtume.

TAMATI

Usomapo Agano Jipya, katika kutafuta kufahamu mtume ni nani na kazi wanayohusika nayo ni gani, utapata kufahamu mambo mengi. Mafundisho mengi yake Yesu yaliwalenga mitume. Mafundisho kwa njia ya nyaraka zamtume Paulo kuhusu huduma ziliwalenga mitume. Agano Jipya liliandikwa na mitume ama wale waliokuwa watenda-kazi pamoja na hao mitume kama Luka. Kitabu cha Matendo ni Matendo ya Mitume.

Bwana Yesu, Kichwa cha Kanisa, analirejesha karama ya huduma ya mtume kwenye kanisa ulimwenguni kote. Kule kulikamilisha kanisa kunaendelea ili Bwana aweze kuleta uvuvio wa nyakati za mwisho katika kila taifa. Mto utatiririka, lakini hadi misingi iwe imara na kuwekwa vizuri, sawa sawa na Neno na Mungu na sio kulingana na desturi za kidini.

Wakati wale mia na ishirini walipokusanyika katika chumba cha juu baada ya Yesu kupaa juu mbinguni, Biblia inasema, ***"Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali"*** (**Matendo1:14**). Kutokana na kujitolea katika kusali, Petro aliongozwa kulijaza lile pengo lililoachwa na Yuda, ambaye kwa wakati huu alikuwa amekwisha kujitia kitanzi. Wakati ambapo msingi wa mitume utakapo wekwa vizuri, basi Siku ya Pentekoste "***itatimia***!"

Bwana alikuwa akiliweka kanisa kwenye mpango ili liweze kupokea kuja kwa Roho mtakatifu bila kikomo.

Ni nani basi alikuwa akiwekwa kwenye mpango? Mitume, huduma ya msingi wa kanisa. Bwana anatuonyesha kwamba mitume wamewekwa kanisani (**1Kor.12:28**); wao ni wa kwanza! Wao ni huduma ya msingi ambapo wengine wote wanajengwa juu yake. Lazima tuwapokee mitume, maana kanisa linapowapokea mitume, linampokea Yesu Masihi na katika kumpokea Yeye, wanampokea Baba Mungu!

Uvuvio mkuu wa nyakati za mwisho tayari umeanza kujithihirisha katika mataifa mbali mbali.

Ni wakati: wakati wa mitume kuwekwa sawa sawa ili Roho Mtakatifu amwagike ambaye atawaguza wote wenye mwili (Yoel 2:28);

Ni wakati wa mto wa Mungu unaotiririka kutoka kwenye kiti cha Enzi cha Mungu (Ufu.22:1), kutok chini ya kizingiti cha nyumba kwa njia ya mashariki (Ezek.47:1), ukianza kuelekezwa juu ya mawe ya msingi yaliyokuwa yamewekwa na Bwana. Ndipo Injili hii ya ufalme itakapohubiriwa ulimwenguni kote kama ushuhuda kwa kila taifa (**Mt.24:14**); Injili itahubiriwa kila kiumbe ishara zikifuata (**Mk.16:15-18**).

SURA YA 3

KARAMA YA HUDUMA YA NABII

Efe.4:11 '*Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii, na wengine kuwa wainjilisti, na wengine kuwa wachungaji na waalimu.'*
Katika kipindi hiki tunaangazia karama ya huduma ya Nabii.

YESU NI NABII

Katika **Kumbu 18:15&18** Musa alitabiri kuhusu kuja kwake nabii ambaye Mungu atakayemleta miongoni mwa waisraeli. BWANA akamwambia Musa, ***"Nitaweka maneno yang katika kinywa chake, Naye atanena yote ninayomwamuru kuyanena kwao."*** **Yoh. 7:40** ***"Hakika huyu ndiye nabii Yule."*** Yohana Mbatizaji alimtambua aliponena kumuhusu Yesu katika **Yoh. 3:34** ***"Kwa kuwa yeye aliyetumwa na Mungu hunena maneno ya Mungu."*** Nabii huyanena maneno ya Mungu.
Maandiko mengi Matakatifu katika Agano Jipya yananena kuwa Yesu ni nabii: **Matt.21:11** ***"Makutano wakasem, 'Huyu ni Yule nabii, Yesu wa Nazareti ya Galilaya.'"***
Nabii atatambuliwa na watu wa Mungu. **Lu.24:19** ***"Wakamwambia, mambo ya Yesu wa Nazareti, aliyekuwa mtu nabii, mwenye uwezo katika kutenda na kunena mbele za Mungu na watu wote.'"***
Nabii anatambulikana kwa ishara na miujiza na kwa ukweli wa Maneno ambayo ananena.
Yoh.4:19 ***"Yule mwanamke akamwambia, Bwana, naona ya kuwa u nabii.'"***

Nabii anatembea katika karama za Roho, (**1Kor.12:8-10**).

MANABII WA AGANO LA KALE

Manabii wengi walijitokeza katika Agano la Kale na kunena kwa niaba ya Mungu. BWANA alinena moja kwa moja kupitia kwao.
Yeremiah 1:4 ***"Neno la BWANA lilinijia, likisema, …"***
Isaya 6:8-9a ***"Kisha nilisikia sauti ya BWANA, akisema; 'Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.'Naye akaniambia, Enenda, ukawaambie watu hawa …'"***
BWANA alinena na taifa asi la Israeli kwa njia ya nabii Ezekieli. **Ezek.2:4** ***"Mimi nakutuma kwa hao; nawe utawaambia, Bwana MUNGU asema hivi.'"***

TAFSIRI:
Nabii
Nabii: Yule anayenena wazi, anayeelezea habari njema ya Mungu, linaashiria kama mkalimani wa mausia ya miungu katika lugha ya Kiyunani.
Katika maandishi ya zamani ya asili ni tafsiri ya neno *'roeh'* Mwonaji; **1Sam.9:9**, kuashiria kuwa nabii alikuwa na uhusiano wa haraka ama karibu na Mungu. Pia linatafsiri neno *'nabhi',* maana yake yule ambaye ujumbe wa Mungu unajitokeza kwa njia yake ama yule anayejulishwa siri. Hata hivyo, kwa ujumla, nabii alikuwa ni Yule ambaye Roho wa Mungu alikuwa juu yake, **Hesabu.11:17-29**, Yule ambaye kwa yeye na kwa njia yake Mungu hunena, **Hesabu.12:2; Amos 3:7-8**. Katika hali ya Agano la Kale jumba za manabii zilikuwa kwa upana matangazo ya makusudi ya wokovu na utukufu utakaotimizwa siku za baadaye; utabiri katika Agano Jipya ulikuwa wa kuhubiri juu ya ushauri wa neema ambayo tayari imetimizwa na utabiri wa makusudi ya Mungu siku za usoni.

NABII ANA

Mtu wa kwanza kuitwa nabii katika Agano Jipya ni mwnamke anayeitwa Anna.
Luka 2:36-38 yatwambia kuwa Ana alikuwa nabii. Maandiko matakatifu yanaelezea kuzawa kwake na kabila. The Scripture gives her genealogy and tribe. Anapewa umuhimu na wasifu kwa kuwa alikuwa nabii; ana huduma ya nabii. Biblia tena inatoa maelezo zaidi kuhusu majikumu na hali yake: alikuwa mjane kwa karne nyingi na alijitolea kwa kumtumikia Mungu, ***'haondoki katika hekalu'*** **(aya ya 37);** kwa maneno mengine aliutumia wakati wake wote mali pa uwepo wa Mungu, akimtumikia, ***'kwa kufunga na kusali usiku na mchana.'*** Alijitolea kwa Mungu; alijua mahali pa maombi na kufunga katika uhusiano wa karibu; alidumu katika Uwepo wake.

Ana alikuwa mwanamke mkongwe, alikuwa na miaka mingi katika huduma, alikubalika kama nabii na alitumia muda wake mwingi katika kufunga na kuomba hekaluni, katika Uwepo wa Mungu. **Alijitolea na kumcha Mungu.** Kupitia kwa kuomba na kufunga, alikaa karibu na uwepo wa Mungu, **huduma yake ya unabii ilikuwa kunena juu ya Bwana na kunena juu ya kusudi Lake la Ukombozi**. Kwa sababu Ana anamjua BWANA; hakukosa kujua siku ya kutembelewa kwake.
a.38 ***'Huyu alitokea saa ile ile akamshukuru Mungu, na wote waliokuwa wakitarajia ukombozi katika Yerusalemu akawatolea habari zake.'*** Ana alinena habari za BWANA; huu ulikuwa ndio utabiri wake, kunena juu ya BWANA na kazi yake ya ukombozi. Anatoa shukrani zake hadharani anapoitambua siku yake ya kutembelewa; anamtambua MASIHI. Hatulii ila anamtukuza BWANA, Mungu wa Israeli.

UREJESHO WA KARAMA YA NABII

Siku hizi za mwisho, Mungu anarejesha karama ya huduma ya nabii. Wanaume kwa wanawake wanaendelea kukuzwa wakiwa na ufahamu wa maandiko kuhusu unabii, wakifundisha na kuhubiri ***"neno kwa majira",*** wakifungua maandiko **(Luka 24:27)**, na kuwakumbusha watu wa Mungu ***"katika kweli waliyo nayo"*** **(2 Petor 1:12).** Haya ni bayana ya mambo ambayo nabii anastahili kuyatenda katika huduma yake ya kuhubiri. Nabii anayafungua maandiko matakatifu katika ufahamu wa kweli waliyonayo.
Tunawezaje kuthibitishwa katika kweli tuliyonayo? Tunathibitishwa wakati ambapo mtu anaendelea kutuleta kufahamu: kwa njia ya mahubiri na mafundisho: kupitia kwa Maandiko Matakatifu yanapofunuliwa na tunapokea ufunuo kwamba 'hili ndilo Mungu analosema'.

'UKWELI TULIO NAO' NI GANI?

Neno la sasa: neno ambalo Mungu anasisitiza sasa. Biblia nzima ni Neno la Mungu, lakini ni nini anasema hivi sasa? Roho anasema nini kwa kanisa sasa ambalo litawezesha kanisa kushinda ikiwa litasikia Neno na kulitii, jinsi Yesu alivyoyaa katika **Ufu: 2&3**? Ni nyaraka za unabii. Yesu anasema kuwa ikiwa kanisa litasikia yale Roho analiambia kupitia kwa nyaraka, litakuwa la ushindi. Tunasikia Neno la unabii la Mungu na hilo ndilo Neno tunalostahili kulitii. Neno linalotoka kwa BWANA sasa!
'Ukweli tulio nao' ambao Mungu anataka tuthibitishwe nao sasa: **Mungu anawakamilisha watu wake ili waweze kuuthibiti uwepo Wake.** Anawaita watu Wake kuendelea na kuufikia utimilivu.

MUNGU ANAIREJESHA KARAMA YA NABII!

Yeremia 1:5 Mungu anasema '***kabla sijakuumba katika tumbo nalikujua, na kabla hujatoka tumboni, nalikutakasa; nimekuweka uwe nabii kwa mataifa.'***
a.6 '*Ndipo niliposema, Aa Bwana MUNGU! Tazama siwezi kusema; na mimi ni mtoto'.*

a.7 – 8 '*Lakini BWANA akaniambia, usiseme, mimi ni mtoto, maana utakwenda kwa kila mtu nitakayekutuma kwake, nawe utasema kila Neno nitakalokuamuru. usiogope kwa sababu ya hao maana mimi nipo pamoja nawe nikuokoe, asema BWANA"'
a.9 – 10 '*Ndipo BWANA akaunyosha mkono wake, akaniguza kinywa changu; BWANA akaniambia.'"*

1) ***"Tazama nimetia maneno yangu kinywani mwako.***
2) ***tazama nimekuweka leo juu ya mataifa na juu ya falme;***
3) ***ili kung'oa na kubomoa, na kuharibu, na kuangamiza;***
4) ***ili kujenga na kupanda."'***

Hizi sehemu za huduma ya nabii ziko zinarejeshwa.

NENO LAKE MUNGU NI LA UNABII NA LINAFAA KUFUNDISHWA KATIKA UFAHAMU WA KIUNABII

2 Petro 1:19-21 '*Nasi tuna Neno lile la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu; mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu Fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.'*

Neno la Unabii linatakiwa likubaliane na Maandiko Matakatifu. Ndoto au maneno ambayo watu wanapokea yanatakikana kuthibitishwa na Neno la Mungu. Mtu aliye na karama ya huduma ya nabii anaweza kuligawanya neno la kweli ipasavyo kiunabii.

Ana, nabii, **alitambua siku ya kujiliwa**: tunahitaji sauti ya nabii leo ili tusikose kujua siku na nyakati za kujiliwa.
Ana alitambua kuja kwake Masihi: tunawahitaji manabii kunena kwa niaba ya BWANA na kurejea kwake hivi karibuni, leo.
Mungu anaikusa huduma hii ya nabii kwa kusudi hili: kuanda kanisa kwa ajili ya kurejea kwake, na kuliongoza kanisa kwa ufunuo unaotokana na Neno lake kupenyeza giza na kuleta siku ya nuru kulashiria kurejea kwake ***(Isaya 60:1-3).***

AGABO NABII.

Matendo 11:27-30.

a.27 *'manabii walishuka kutoka Yerusalemu kuelekea Antiokia'*
tayari huduma ya nabii inatambulika katika kanisa la Agano Jipya. Manabii walishuka kutoka kwa kanisa moja (Yerusalemu) kuelekea kwa linguine (Antiokia) – wanakubalika na kutambulika kama huduma ya karama kwa Mwili wa Kristo. Nabii anaenda mahali ambapo Mungu anamwelekeza kwenda.

a.28 Agabo ndiye anayeangaziwa hapa. ***'Alionyeshwa na Roho kwamba kutakuwa na njaa kubwa ulimwenguni kote'.*** Alipokea maono; alionyeshwa kitu. Nabii hakufungua maandiko Matakatifu hapa! Anatabiri, matukio ya siku za usoni, kama maonyo, ama jambo linalo stahili kushughulikiwa. Nabii anawezeshwa kutabiri sawa sawa na vile Roho anavyoonyesha.

NI NINI MTIHANI WA NABII
Kumbu 18:18 – 22

1. **a.18 *'Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwanndugu zao mfano wako wewe, name nitatia maneno yangu katika kinywa chake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru.'***
2. Mungu ndiye anayetia maneno katika kinywa cha nabii.
   a.15 *'BWANA Mungu wako, atakuondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zako kama nilivyo mimi, msikilizeni yeye.'*

3. Neno lake nabii linafaa kuaminika, kama Neno lake Mungu Mwenyewe.
   a.20 ***'Lakini nabii atakayenena Neno kwa kujikinai kwa jina langu, ambalo kulinena au atakayenena kwa jina la miungu wengine, nabii Yule atakufa.'***
4. Wengine wanatabiri kwa kujikinai lakini hawakusikia kutoka kwa Bwana, ama wanaongozwa na miungu wengine.
   a.21– 22 ***'Nawe ukisema moyoni mwako, Tutajuaje Neno asilosema BWANA? Atakaponena nabii katika jina la BWANA, lisifuate jambo lile wala kutimia, hilo ndilo Neno asilolinena BWANA; kwa kujikinai amelinena huyo nabii, usimwogope.***
5. Kile ambacho nabii wa kweli anatabiri hakika kitatimia; bila hiyo watakuwa wamenena kwa kujikinai.

Maandiko Matakatifu yanatwambia neno lake Agabo lilikuwa la kweli; njaa ilitukia wakati wa utawala wa kaesaria Klaudio.

Matendo11:29 Na wale wanafunzi wakaazimu, baada ya kupokea neno lake nabii. ***'kila mtu kwa kadiri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi.'***
a.30 ***'Wakafanya hivo'*** – Neno lilitekelezwa, na msaada ukatumwa kwa mikono ya wazee wawili Barnaba na Sauli kwa wazee walioko Yerusalemu.

Huduma ya nabii ni huduma wazi, japo karama ya unabii ni hadhara, wakati wote huwa miongoni mwa mashahidi wengi, wazee wakijumuishwa ikiwezekana, ili unabii huo uchunguzwe, upimwe na uthibitishwe.
1 Kor.14:29 ***'na manabii wanene wawili au watatu, na wengine wapambanue.'***
Acha ikiwezekana, kutoa maneno ya binafsi kwa watu binafsi wakati hakuna mtu mwingine. Usilazimishe maneno kwa mtu yeyote. Fahamu muongozo wa Biblia na mipaka ya karama na huduma.

Katika **Matendo 21:10–14** Agabo, nabii, tena anatabiri, kuhusu yale yatakayo mpata Paulo.
a.8 Paulo pamoja na msafara wake walikuwa waki kaa kwake Filipo, muinjilisti.
a.9 Filipo ana binti wane walikuwa na kipawa cha unabii. Tunabaini kuwa hii ni karama ya unabii. Hawa binti hawaja semekana kuwa walikuwa manabii.
a.10 Agabo anajulikana kuwa nabii haswa.
a.11 Alinena kutokana na Roho Mtakatifu, ***'Hivi asema Roho Mtakatifu.'***
a.12 wote waliokusanyika waliamini Neno lake Nabii, Neno lake Roho Mtakatifu kupitia kwa nabii.
a.13 Lakini Paulo tayari anafahamu hatari inayomngojea Yerusalemu, tazama **Mate 20:22 – 23.**
a.14 Alikubaliana na ukweli wa Neno, lakini lilikuwa la kuthibitishwa, bali halikumzuia kuendelea na safari yake, na msafara wake ulikubaliana naye kwa kusema, **'*Mapenzi ya BWANA yatendeke'***

MAMBO YANAYOONYESHA NA KUTULINDA KUTOKANA NA UNABII WA KIBINAFSI:

1. Neno la kuthibitika wala sio la kubuni; huduma ya unabii sio ya kubuni mambo mapya katikamaisha, bali kuthibitisha yale ambayo Mungu tayari amekuonyesha.
2. Mtu aliyeleta neon la unabii alikuwa wa kuaminika; Agabo alikuwa muhuduma aliyekuwa ametambulikana kwa karama hiyo, na kuthibitika;

3. Maneno ya binafsi yasikuelekeze katika njia ya kukuongoza. Paulo hakubadili mipango yake.
4. Unabii wote ni katika sehemu tu (**1 Korintho 13:9**) na mara nyingi huingia katika mipango mikubwa ya Mungu;
5. Mashahidi walikuwepo kubainisha Neno hilo;
6. Kukubaliana na Neno hilo haimaanishi kuwa kipofu ama kukubaliana kwa haraka.

MANABII WENGINE KATIKA CHUO CHA MATENDO YA MITUME

Katika **Matendo 15:22,** Yuda pia, aliyeitwa Barsaba, na Sila wanatajwa kama viongozi miongoni mwa wandugu. Pia wanatajwa katika aya **ya. 32**, ***"Tena Yuda na Sila wenyewe ni manabii, wakawausia ndugu kwa maneno mengi, wakawathibitisha."*** Hawa walikuwa viongozi wakiwa manabii: karama yao ya uongozi ilikuwa ya unabii. Walitumia karama yao kutia nguvu na kuwausia na kuwatia nguvu ndugu. Karama ya huduma ya nabii inatakikana kutia nguvu, kuusia na kuwajenga wandugu.

MAFUNDISHO ZAIDI KUHUSU NABII

Matt. 10:41 anatupatia msingi wa kuweza kumpokea nabii; ***"Ampokeaye nabii kwa kuwa ni nabii, atapata dhawabu ya nabii."***

Matt. 13:57 Yesu akawaambia, ***"Nabii hakosi kupata heshima, isipokuwa katika nchi yake, na nyumbani mwake mwenyewe."***

TUNAWEZAJE KUPOKEA NENO LA UNABII?

Manabii wanatakiwa wakaribishwe katika kunena katika mkutano wa kanisa,

1 Kor.14:29 ***"Na manabii wanene wawili au watatu, na wengine wapambanue."***

a.30 ***"Lakini mwingine aliyeketi akifunuliwa neno, Yule wa kwanza na anyamaze."***

a.31 ***"Kwa maana ninyi nyote mwaweza kuhutubu mmoja mmoja, ili wote wapate kujifunza, na wote wafarijiwe."***

Tunaweza kujifunza kwa sikia unabii. Wawili au watatu wakinena inaweza kupanua na kuleta ufahamu wa kina kwa kile ambacho Mungu anasema.

a.32 ***"Na Roho za manabii huwatii nabii."*** Karama iko chini ya utawala wa nabii. Ikiwa unaneno na unajua linatoka kwa Bwana, omba nafasi ili uweze kushiriki. Nabii anatakikana kuleta ujumbe ambao Bwana anampa; yeye hausiki kwa vyo vyote vile jinsi ujumbe huo utakapo pokelewa au kuitikiwa.

a.37–40 ***"Mtu akijiona kuwa nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana. Lakini mtu akiwa mjinga, na awe mjinga. Kwa ajili ya hayo, ndugu, takeni sana kuhutubu, wala msizuie kunena katika lugha. Lakini mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu"***

MUNGU AMEWEKA KILA HUDUMA MAHALI PAKE

1Kor.12:18 ***"Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka."*** Ni Mungu ndiye aliyeweka kila kiungo mahali pake katika mwili. Mungu anajenga kanisa lake. Anatuweka mahali anajua tunafaa.

1 Kor.12:28 ***"Na Mungu ameweka wengine katika kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za kuponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina mbali mbali za lugha."***

Efe.2:20-22 ***"Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni Jiwe Kuu la Pembeni. Katika yeye jingo lote linaungamanishwa vema na kukua hata liwe hekalu takatifu katika Bwana. Katika yeye ninyi nanyi mnajengwa pamoja kuwa maskani ya Mungu katika Roho."***

Watu wanapozidi kuungamanishwa katika nyumba hii, wanajengwa kwa misingi ya mitume na manabii. Huu ndio msingi wa Biblia na kama umewekwa vizuri mahali pake, nyumba itakuwa imara.

MUNGU ANAFUNUA SIRI ZAKW KWA MITUME NA MANABII

Efe.3:2-3 ***"ikiwa mmesikia habari ya uwakili wa neema ya Mungu niliyopewa kwa ajili yenu; ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache…";***

a.5 ***"siri hiyo hawakujulishwa wanadamu katika vizazi vingine; kama walivyofunuliwa mitume wake watakatifu na manabii zamani hizi katika Roho."***

Hawa ni manabii wake Yesu Aliyepaa. Manabii wa Agano la Kale mara nyingi walitabiri kuhusu siri hii bali hawakuelewa kile ambacho walikuwa wakinena kwa sababu haikuwa wamefunuliwa. Walitamani kuiona siku kama ya leo. Mungu sasa amefunua siri hii kwa Roho Mtakatifu kwa mitume na manabii wake watakatifu.

TAMATI

Huduma ya nabii na karama zile zingine nne, zilitolewa na Yesu ni mwito kutoka kwa Mungu kwa kanisa. Zimetolewa kwa kusudi la kujenga na kuwakamilisha watakatifu (maana kila mtu amepewa neema kulingana na kipawa cha Kristo) **(Eph.4:7).**

Inawezekana mtu mmoja kuwa na zaidi ya karama moja. Kwa mfano, Paulo - Mhubiri, mtume na mwalimu … (**2Tim.1:11)**

Katika hali ya nabii, na kipawa cha kutabiri (**1Kor.12:10**) mara nyingi huambatana na huduma ya nabii, ila katika njia kubwa. **Nabii ndiye anayetabiri na pia kunena**. Kwa maneno mengine, kuna mahubiri na mafundisho ya kinabii, bali nabii anawezeshwa kwa Roho Mtakatifu kutabiri matukio, matendo na kutoa mwelekeo wa kiroho kwa kanisa na watu binafsi katika Mwili wa Kristo.

SURA YA 4

KARAMA YA HUDUMA YA MUINJILISTI.

Efe.4:11 ***"Naye alitoa wengine kuwa mitume, wengine kuwa manabii, wengine kuwa wainjilisti, wengine kuwa wachungaji na waalimu."***

Muinjilisti.

Ezek. 34:5-6 ni aya za msingi ambapo Bwana anathihirisha moyo wake mwenyewe kwa ajili ya uinjilisti, ***"Nao wakatawanyika, kwa sababu hapakuwa na mchungaji; wakawa chakula cha wanyama –mwitu, wakatawanyika. Kondoo zangu walitanga-tanga katika milima yote, na juu ya kila kilima kirefu; naam, kondoo zangu walitawanyika juu ya uso wote wa dunia; wala hapakuwa na mtu aliyewauliza, wala kuwatafuta."*** Watu wa Mungu walikuwa wametawanyika wala hapakuwa na mtu aliyewatafuta. Hiki ni kilio cha moyo wa muinjilisti.

Katika kitabu cha **Efeso sura ya Nne.4**, tuna karama tano za huduma ambazo Yesu alitoa kwa ajili ya kanisa. **Mtume na nabii ni huduma za msingi.** Hizi huduma hufanya kazi nyuma ya pazia, zikiweka misingi na kuinua huduma zingine. **Huduma zile ambazo ziko juu ya ule msingi, kwanza ni muinjilisti ambaye hukusanya, halafu mchungaji ambaye hutunza na kuchunga, hatimaye mwalimu ambaye huleta Neno la kusitawisha waaminio katika Neno la Mungu.**

Katika **Ezekiel**, Mungu anasema: 'kwa sababu huduma ya uchungaji, huduma ya kuchunga imezembea, watu wake Mungu wametawanyika wala hapana mtu aliyewatafuta. Wakati Yesu alipokuja alisema, ***"Kwa kuwa Mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea,"*** **Lu.19:10.** Alisema kuwa alitumwa haswa kwa wna-kondoo wa nyumba ya Israeli waliopotea.

Kupitia kwa kufa na kufufuka Kwake,
alitoa huduma ya uinjilisti kwa ajili ya mataifa yote.

Ezek.34:11 ***"Maana Bwana MUNGU asema hivi; Tazama, mimi mwenyewe, naam, mimi, nitawatafuta kondooo zangu, na kuwaulizia."***
a.13 ***"Nami nitawatoa katika watu wa mataifa, na kuwakusanya katika nchi zote, nami nitawarudisha katika nchi yao wenyewe, nami nitawalisha juu ya milima ya Israeli, kando ya mifereji ya maji; na katika mahali pote pa nchi panapokaliwa na watu."***
a.16 ***"nami nitawatafuta waliopotea, nitawarudisha waliofukuzwa, nitawafunga waliovunjika, nitawatia nguvu wagonjwa; noa wanono na wenye nguvu nitawaharibu."***

Katika **Luka 15,** Yesu anatoa hadithi juu ya mchungaji aliye na kondoo 100, 99 wako salama katika kundi bali mmoja amepotea. Katika moyo wa mchungaji wa kweli mna huduma ya uinjilisti, ya kukusanya waliopotea na kuwahudumia wokovu.

Kuwakusanya watu wa Mungu ni uinjilisti. Ni huduma ya muinjilisti kwenda kuwatafuta waliopotea. Huduma ya uinjilisti hufanya kazi kwa karibu sana na huduma ya mchungaji.
Kuna **makundi mawili ya watu ambao wanahitaji kufikiwa:** watu wa Mungu ambao bado hawajasema 'NDIO', na watu wa Mungu ambao wametoroshwa.

YESU NDIYE MUINJILISTI

Yesu alitumwa kwa nyumba ya kondoo wa Israeli waliopotea. Alijua kwamba aliitwa kuwafikia waliopotea. **Matt.15:24** ***"Akawajibu akawaambia, 'Sikutumwa ila kwa nyumba yakondoo wa Israeli waliopotea.'"*** Yesu alichikuwa muda Wake mwingi kutoka sehemu

moja hadi nyingine akihubiri kuhusu ufalme wa Mungu. Tunaona mpango wake wa kuhama hama katika kazi ya uinjilisti katika huduma ya Yesu.
Marko 1:38 ***"Akawaambia, Twendeni mahali, mpaka vijiji vilivyo karibu, nipate kuhubiri huko nako; maana kwa hiyo nalitokea.'"***

Huduma ya kuhubiri ni huduma ya muinjilisti, kuwahubiri injili waliopotea. Yesu akasema katika **Marko 16:15** wakati aalipokuwa akiwatuma wanafunzi wake kwenda nje, ***"Enendeni, basi, ulimwenguni kote mkaihubiri injili."*** Walioamini wanafundishwa Neno ila kuhubiri ni kwa ajili ya wale waliopotea. **Lu.4:43** ***"Akajibu akasema, 'Imenipasa kuihubiri habari njema ya ufalme wa Mungu katika miji mingine pia; maana kwa sababu hiyo nalitumwa.'"*** Lazima habari njema ihubiriwe katika kila mji na miji mikuu.
Kanisa kihistoria limezingatia mahubiri kanisani kinyume na vile Maandiko Matakatifu yanavyoshuhudia kwamba tuwahubiri habari njema walio masikini wa roho, ili kwamba wakaweze kutajirika. Naam, mahubiri yanaweza kutendeka katika majengo ya kanisa, bali kuhubiri kulingana na Maandiko Matakatifu na kihistoria katika vuvio kuu kama ile ya Wesley katika karne ya 18, ni katika mahali pa hadhara mijini, bustanini, sokoni, uwandani, nje ya malango ya viwanda.

UINJILISTI NI HUDUMA YAKE YESU ALIYEPAA **(Efe.4:11).**

Huduma ya muinjilisti ni dhihirisho la nguvu la Yesu aliyefufuka katika kanisa Lake. Filipo anaitwa ***"muinjilisti"*** katika **Matendo 21:8**. Kutajwa kwake mara ya kwanza ni katika **Matendo 6:5** ambapo alikuwa miongoni mwa wale waliochaguliwa kwa ajili ya mgao wa kila siku wa chakula kwa wajane**, (a.1-3**). Kulihitajika mambo matatu muhimu yaliyo wazi katika maisha ya wale waliochaguliwa (**a.3): -**

1. **Walioshihudiwa kuwa wema**
2. **Waliojawa na Roho Mtakatifu**
3. **Watu wenye hekima**.

Filipo alihitimu na akachaguliwa. Kazi yake ya kwanza ilikuwa ya utumishi, kushughulikia mambo ya meza, awe msaidizi. Alichaguliwa na kutengwa kwa ajili ya huduma kwa kuwekewa mikono na mitume, (**Matendo 6:6**). Kuhudumu kama msaidizi ilikuwa shule nzuri ya mafunzo kwake kuwa muinjilisti**. 1Tim. 3:13** ***"Kwa maana watendao vema kazi ya shemasi hujipatia daraja nzuri, na <u>ujasiri mwingi katika imani</u> iliyo katika Kristo Yesu."***
Muinjilisti anahitajika kuwa na ujasiri!
Katika **2Tim.4:5** Paulo anamwambia **Timotheo** ***"Bali wewe, uwe na kiasi katika mambo yote, vumilia mabaya, fanya kazi ya muhubiri wa injili, timiza huduma yako."*** Timotheo ni mtume, lakini anatakiwa afanye kazi ya uinjilisti.
Amri ya Yesu inayokaribia huduma ya uinjilisti ni katika **Luke 24:48&49** ***"Nanyi ndinyi mashahidi wa mambo haya. Na tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu",*** na latika **Matendo 1:8** ***"nanyi matakuwa mashahidi wangu ….. na ulimwenguni kote".***
Kushuhudia imani ni kazi ya uinjilisti.

MUINJILISTI

Muinjilisti: **<u>ni Yule ambaye ametumwa na ujumbe, au mjumbe anayeondoka na kwenda nje</u>**.
Katika **Matendo 8:4** ***"wale waliotawanyika walienda kila mahali wakilishuhudia lile Neno".*** Walikuwa wakifanya kazi ya uinjilisti. **a.5** ***"Filipo akatelemka akaingia mji wa Samaria, akawahubiri Kristo".*** Ni ajabu kwamba wanafunzi hawakuingia Samaria kwa hiari, hata baadaye (**Matendo 10**) Petro anahitaji Mungu kuingilia kati ili aweze kuwaendea Mataifa. Yesu alikuwa amawaamuru wanafunzi wake kumushuhudia Samaria katiuka

Matendo 1:8. Filipo alihubiri na miujiza ikatendeka: **Matendo 8:7** ***"Pepo wachafu wakawatoka wengi waliopagawa nao, wakilia kwa sauti kuu; na watu wengi waliopooza, na viwete wakaponywa."*** Hili lilileta furaha kubwa (**a 8**.)

Tunda la mahubiri na huduma yake Filipo katika ishara na maajabu ni kufanya mapinduzi makamilivu dhidi ya ngome za mapepo ya mpinga-kristo katika mji, ambayo hujithihirisha kupitia kwa watu wenye mamlaka, Simioni Yule mchawi, akipoteza uweza wake juu ya mji huo, (**Matendo 8:9-13**). **Matendo 8:14–17** Mitume, Petro na Yohana walitumwa kutoka Yerusalemu wakati ambapo kanisa la Yerusalemu liliposikia ushuhuda kutoka Samaria. Petro na Yohana walitumiwa kuwekea Roho Mtakatifu kwa walioamini wachanga. Tambua kwamba muinjilisti hakutumiwa kikamilifu kuweka msingi wa kanisa hili change; ndiposa mitume walitumwa huko.

MUINJILISTI ANAFANYA KAZI GANI?

Matendo 8:26 ***"Malaika wa Bwana akasema na Filipo, akamwambia, Ondoka ukaende upande wa kusini hata njia ile itelemkayo kutoka Yerusalemu kwenda Gaza; nayo ni jangwa.'"***

Filipo aliitwa na Bwana aondoke katika mkutano mkuu wa uvuvio samaria ili aende amuhubirie mtu mmoja! KWA NINI? Kwa sababu Filipo alikuwa muinjilisti.

<u>Tabia ya Muinjilisti</u>

1. **Kila nafsi ni ya umuhimu kwake**
2. **Muinjilisti anaenda kule ambako Roho Mtakatifu anamtuma kwenda.**
3. **Muinjilisti ana muhubiri Yesu, Matendo 8:35** ***"Filipo … akianza kwa andiko lilo hilo, akamuhubiri habari njema za Yesu."***
4. **Muinjilisti analeta ujumbe wa wokovu na ufalme wa Mungu,** ambao huleta toba, imani na ubatizo. (**Matendo 8:36-38**).
5. **muinjilisti husafiri hadi maeneo mengine.** Yeye huondoka akiwa na ujumbe kwa sehemu zingine na watu kama anavyoongozwa na Bwana, (**Matendo 8:40**).

Wainjilisti ni wavuvi wa nafsi; wainjilisti ni wavunaji.

KUVUNA NAFSI ZA WATU

Ni wakati wa kuvuna nafsi za watu! Watu wengi wametosheka na "kupanda mbegu", wakitumaini kwamba mtu mwingine atakuja kuvuna. Bwana anawaita watenda kazi kwa ajili ya mavuno kwa sababu ni wakati wa mavuno. **Luka 10:2** ***"Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache; basi mwombeni Bwana wa mavuno apelike watenda kazi katika mavuno yake."***

Bwana anawatuma watenda kazi katika mavuno: ni katika mavuno Yake. Amekuwa akitunza kutoka upanzi wake na kukuwa pia.

Kuvuna kunamaanisha kuleta miganda: Zab. 126:5-6 ***"Wapandao kwa machozi watavuna kwa makelele za furaha. Ingawa mtu anakwenda zake akilia, azichukuapo mbegu za kupanda, hakika atarudi kwa kelele za furaha, aichukuapo miganda yake."***

Machozi ni machozi ya maombezi, miganda ni nafsi. Maombezi ni muhimu kwa uinjilisti unaofanyakazi.

Wakati wa mavuno ni wakati ambapo magugu yanatengwa kutoka kwa ngano (Matt.13:30). Mwisho wa nyakati kutakuwa na mavuno ya watenda maovu na menye haki pia**.**

Maelezo kwa wale wanaovuna

Isaya 28:23-29 Neno la Mungu linatuagiza kwamba Mungu atatuelekeza katika kulima, upanzi na katika mavuno. Katika mfano wa Mpanzi na Mbegu katika **Matt.13:3-9** na Yesu

akifasiri mfano huo katika **a.18-23,** inatoa maelezo zaidi kuhusu hali ya mchanga wa mioyo ya wanadamu. Roho mtakatifu atatuelekeza na kutufundisha jinsi ya kuwa wafunaji wema.

UINJILISTI KATIKA KITABU CHA RUTHU

Ruthu sura ya 2: Tunamwona Boazi, mfano wa Kristo akiangalia kazi ya mavuno**.** Wavunaji ni mfano wa muinjilisti. Ruthu ni mfano wa muinjilisti.

a.4 Boazi, bwana wa mavuno, mfano wa Kristo, alitoka Bethlehemu. Yeye na wavunaji wake walikuwa katika Bwana pamoja.

a.5 bwana wa mavuno anatambua kwamba kuna mvunaji mgeni miongoni mwao wanaookota masazo.

a.6 Mtumishi aliyewasimamia wafanyakazi anamshuhudia kuwa yeye ni nani. Kila mvunaji anajulikana na Bwana.

a.7 Ruthu tayari alikuwa akifanya kazi kwa bidii katika mavuno, lakini alijua kwamba anahitaji kupumzika katika nyumba.

a.8 Boazi anamkaribishi huyu mgeni kuokota masazo katika shamba lake, na kushiriki na wasichana wengine.

a. 9 kuna usalama mahali hapa pa ushirika na maji ya kunywa katika mavuno.

a.10-12 Bwana hubariki uaminifu; Bwana anaona matendo yetu na atatulipa vilivyo; kwa hivyo Ruthu anatunukizwa na Boazi. Ushuhuda wake ulikuwa umemtangulia.

a.14 Boazi anampa mkate na siki; je, huu ni mfano wa meza ya Bwana? Boazi anathibitisha mahali pake katika ushirika.

a.16 Boazi kwa makusudi anammwagia Baraka Ruthu naye anaokota nafaka nyingi! Alimpa nafaka. Bwana huleta nafsi mahali ambapo tutaweza kukutana nao tunapojitolea kufanya kazi katika mavuno. Yeye haitaji tuwe tumehitimu, wavunaji mashuhuri!!

Kuvuna nafaka

Muinjilisti haitaji tu kukusanya nafaka kidogo bali Bwana wa mavuno hupeana miganda ya kukusanywa. Kuna mavuno nyakati za mwisho: mkusanyiko mkubwa wa nafsi katika ufalme wa Mungu. Ruthu ni mgeni, Mmataifa, mtu aliyezaliwa katika kabila lililodharauliwa. Wamoabi walitokana kati ya mbari ya Lutu na binti yakealikuwa mwamini wa kweli. Anakubalika kikamilifu na Bwana; hata kiwango kwamba anataka kumwoa**. Ruthu 3-4**, tambua kwamba baada ya mavuno kumalizika, **kulikuwa na harusi.** Baada ya mavuno ya mwisho wa nyakati, chumba cha karamu ya harusi kitakuwa kimejaa. Yesu na bibi –arusi watafunga ndoa!

MAFUNDISHO ZAIDI KUTOKA KWA MAANDIKO MATAKATIFU KUHUSU WAINJILISTI.

Kitabu cha **Mithali** kina maelezo muhimu kuhusu mwenendo wa wavunaji (wainjilisti).

Mithali.6:6-8 Chungu mwenye bidii hukusanya chakula chake wakati wa mavuno, wakati ambapo mvivu (mtu) analala.

Mithali.10:5 Pia, mvivu analala wakati wa mavuno, wakati ambapo mwenye hekima anakusanya.

Mithali.11:30 yatwambia kwamba ***"… mwenye hekima huvuta roho za watu."***

Mithali.20:4 Mtu mvivu hajajiandaa; kwa hivyo hana mavuno. Ni wakati wa kufanya kazi ya uinjilisti!

MUINJILISTI ANATAKIKANA KUELEWA MAANDIKO MATAKATIFU YANAFUNDISHA NINI KUHUSU MAVUNO.

Katika **Manabii** kuna mifano iliyo wazi kuhusu mavuno:

Isaya 9:3 ***"Umeliongeza taifa, umezidisha furaha yao; wanafurahi mbele zako, kama furaha ya wakati wa mavuno, kama watu wafurahivyo wagawanyapo nyara."***

Kuna furaha katika mavuno! Tunafurahia wakati nafsi zinapomjia Bwana.

Yeremiah 5:24 ***"Bwana huwapa mvua, ya masika nay a vuli katika majira yake. Anatuhifadhia majuma aliyoteua kwa ajili ya mavuno."*** Kama jinsi watu hawakumtambua Bwana wa mavuno siku hiyo, wengi hata sasa wamelala, wameketi kitako na bila mpango, bila kutaka kwenda katika shamba kama alivyoamuru BWANA; kwamba kila siku kuu ilihusiana na mavuno.
Yeremiah 8:20 ***"Mavuno yamepita, wakati wa hari umekwisha, wala sisi hatukuokoka!"*** Mkosi wa ajabu: kukosa wakati wa mavuno! Kukosa wokovu.
Hosea 6:11 ***"Tena, ee Yuda, wewe umeandikiwa mavuno, hapo nitakapowarudisha wafungwa wa watu wangu."*** Ni ***"mavuno yaliyoteuliwa"*** tunayoitiwa kuingia ndani yake! Mateka wanafunguliwa. Mavuno yaliyoteuliwa yanatimiza Siku Kuu ya Mabanda ya nyakati za mwisho. Nafsi nyingi zitaokolewa kutoka kwa kila Taifa, kabila na ndimi.
Yoel 2:23-24 Bwana anaahidi ***"mvua ya masika naya vuli"*** pamoja kuleta mavuno maradufu; ngano (mavuno ya nafaka) na divai mpya na mafuta (mavuno ya matunda). Pentekoste na Mabanda pamoja: mkusanyiko mmoja mkubwa. Haya ndiyo ***"mavuno yaliyoteuliwa"*** wakati wa mwisho. (fananisha na **Yakobo 5:7-8**). Mavuno yaliyoteuliwa ni mavuno maradufu, ama upako maradufu – hatimaye Roho Mtakatifu atamwagwa juu ya wote wenye mwili. Kutakuwa na kuhubiri kwa habari njema ya Yesu ulimwenguni kote.
Yoel 3:13 inaashiria kwamba kuna mavuno ya watenda maovu kwa upande mmoja na mavuno ya wenye haki. Hili linathibitishwa katika mfano wa ngano na magugu (**Matt. 13:24-30**).

BWANA ANAWATUMA NJE WAINJILISTI!

Luka 10:1 ***"Basi, baadaye Bwana aliweka na wengine, sabini, akawatuma wawili wawili watangulie kwenda kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe."***
Mpangilio wa ajabu kuhusu wajibu wa muinjilisti: huduma ya namna ya Yohana Mbatizaji – kuenda mbele ya Bwana, kuandaa kuja kwake tukiwa tayari kuponya wagonjwa na kutangaza injili ya ufalme wa Mungu (aya ya 9) na kutoa pepo (aya **ya 17**).

Uinjilisti wa kusambazwa

Wainjilisti wanatumwa kwenda mwele kabla ya kuja kwa makundi ya mitume. Wanaenda kwa nyumba ya mtu wa amani (**Luka 10:5-7**). Kundi la wainjilisti linaingia katika sehemu na kusambaza injili humo. Hili linafanywa kwa njia mbali mbali: Nyumba kwa nyumba, matembezi, kupeana makaratasi ya matangazo ya injili; kuwaalika katika matukio muhimu kama mipango ya mikutano ya watoto au mikutano ya jamii; kushiriki katika kuona sinema ya Yesu pamoja.

Kufanya kazi ya huduma

Kama mfano katika Matendo 8, muinjilisti hajaitwa kupanda makanisa, bali kuwafua waliopotea. Kundi la mitume linaweza kufwata na kupanda ama kuweka kanisa katika msingi.

Kuandaa Watakatifu

Jukumu la mwinjilisti kama mshiriki wa huduma mara tano ni mara mbili - na vile vile kwenda kuhubiri na kushinda roho, mwinjilisti ana jukumu la kuwapa watakatifu huduma ya uinjilishaji (**Waefeso 4: 11-12**). Hii inafanywa kwa njia kadhaa kama vile semina za mafunzo, kuchukua wafunzo kwenye timu, kuhudumu katika mikutano ya ushirika kuhamasisha kanisa lote kufanya kazi ya uinjilishaji.

Kila uinjilisti wa mshiriki

Kila mhudumu na kila Mkristo anapaswa kufanya kazi ya uinjilishaji. Huu ndio ushuhuda ambao Yesu ameagiza kila mmoja wetu afanye. Tumeitwa ***"kutoa utetezi kwa kila mtu anayekuuliza sababu ya tumaini lililo ndani yako, kwa upole na hofu."*** **(1 Pet. 3:15).**

Imepewa uwezo wa kushuhudia
Roho Mtakatifu hututia nguvu (**Matendo 1:8**) kuwa shahidi. Ishara za **Marko 16: 17-18** ni ishara zinazoambatana na wale wanaoamini. Waumini wanaweza kuwaombea wagonjwa kwa ujasiri, kutoa pepo, kusema kwa lugha mpya na kutarajia ulinzi wa kimungu katika zoezi la kushiriki injili.

Maonyesho ya Nguvu
Kushuhudia injili ni pamoja na kuonyesha nguvu za Mungu kupitia ishara. Injili kwa neno na mafundisho tu sio injili kamili. Injili ina sifa ya nguvu, kwa ishara na maajabu.

Ni wakati wa kuinua Wainjilisti
Kanisa linahitaji kuwasaidia wale walioitwa kwenye huduma ya uinjilishaji, wasiwaone kama wahudumu wa daraja la pili ambao siku moja wanaweza kuwa wachungaji. Kanisa la sasa halipokei wainjilisti kama huduma za zawadi za kupaa. Ni makanisa machache sana yanaajiri wainjilisti. Ni wakati wa kumwomba BWANA wa Mavuno ainue wafanyikazi [wainjilisti] kwa mavuno ya wakati wa mwisho, wote wahudumu walioajiriwa wakati wote na watakatifu wengi na wahudumu wengine wanaofanya kazi ya mwinjilisti.

SURA YA TANO

KARAMA YA HUDUMA YA MCHUNGAJI

Waefeso 4:11 "*Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu."*

Mchungaji

EZEKIELI 34 - MCHUNGAJI WA AINA YA MUNGU

Ezekieli 34 Ni sura ambayo inatupa fundisho kuhusu mchungaji. Asili ya mchungaji ni kuwaendea kondoo waliopotea. Yesu mwenyewe alionyesha haya. Katika kila mchungaji kuna moyo wa muinjilisti.

Ezekieli 34:1-10 inaongea kuhusu **wachungaji wasioshugulika** ambao wamekuwa **wakishulutisha na kutawala,** sio kuliangalia kundi vyema. Mungu anaona kinacho tendeka kwa kundi na hajafurahishwa na wachungaji, **aya 10 "***Bwana MUNGU asema hivi; Tazama, mimi ni juu ya wachungaji; nami nitawataka kondoo zangu mikononi mwao, nami nitawaachisha hiyo kazi ya kuwalisha kondoo; na wachungaji hawatajilisha wenyewe tena; nami nitawaokoa kondoo zangu vinywani mwao; wasiwe tena chakula chao."*
Aya 11 ***"Maana, Bwana MUNGU asema hivi; Tazama, mimi mwenyewe, naam, mimi, nitawatafuta kondoo zangu, na kuwaulizia."*** Mungu mwenyewe atawaendea kondoo zake.

MCHUNGAJI WA KWELI

Aya 14 "*Nami nitawalisha malisho mema, na juu ya milima ya mahali palipoinuka pa Israeli litakuwa zizi lao; huko watalala katika zizi jema, nao watakula malisho mema, juu ya milima ya Israeli."*
Huduma ya mchungaji ni kulisha na kutunza kundi
Aya 15 "*Mimi mwenyewe nitawalisha kondoo zangu, nami nitawalaza, asema Bwana MUNGU".*
Aya 16 ***"Nami nitawatafuta waliopotea, nitawarudisha waliofukuzwa, nitawafunga waliovunjika, nitawatia nguvu wagonjwa; nao wanono na wenye nguvu nitawaharibu; nitawalisha hukumu."***
Huduma ya mchungaji ni kuwatafuta waliopotea na kurejesha waliofukuzwa, kuwafunga waliovunjika, na kuwatia nguvu/kuwatibu wagonjwa.
Ezekieli 34:14-16 kwa mktasari: mchungaji wa kweli –

1. **Hulisha kwenye malisho mema**
2. **Hupatiana malisho mahali juu milimani mfano pahali juu pa Mungu**
3. **Kuna mahali pa kulazwa katika zizi, kulazwa mahali pema**
4. **Mchungaji mwema anawatafuta waliofukuzwa na kuwarejesha**
5. **Kuwafunga waliovunjika na kuwatia nguvu wagonjwa na kuwatibu**

BWANA NDIYE MCHUNGAJI

Katika **Zaburi 23:1-6** Huduma ambayo anaifanya Bwana aliye mchungaji inafafanuliwa zaidi.

1. Zaburi 23:1 Mahitaji yote yanashughulikiwa
2. Picha ya malisho mema kwa chakula na pa usalama pa kulazwa
3. Matibabu/ urejesho wa nafsi, kuongozwa kwa njia za haki
4. Ulizi na faraja katika maovu, shinda na kifo
5. Meza kuandaliwa (pengine meza ya BWANA) na upako mbichi wa kukuwezesha kushinda adui
6. Kuna hatima na tumaini la kondoo wa BWANA

Hukumu ya wenye nguvu waliowadhurumu wanyonge
Ezekieli 34:17-22 BWANA awahukumu kondoo ambao wamekuwa na ubinafsi na kuwadhurumu walio wanyonge.
Mchungaji atainuliwa
Aya 23-31 anazungumzia kuinuliwa kwa mchungaji ambaye atawalisha na kuwaangalia kondoo.
Hii inazungumza kumhusu Yesu. Yohana 10:1-18 ni utimilifu wa aya hayo katika **Ezekieli.**
Agano la amani
Ezekieli 34:25 anazungumza kuhusu agano la amani; wanyama wakali wa jangwani, [wanyama wa kipepo] watakomeshwa na kutakuwa na usalama.

ZIZI ZITAKUWA NI MAHALI PA BARAKA
Aya 26 zizi patakuwa mahali pa baraka; manyunyu ya Baraka yatashuka.
Aya 27 nchi itatoa mazao yake, matunda, nafaka na uhuru.
Aya 29 nitawainulia miche; linganisha na **Malaki 3:12**
Aya 31 sisi, wanadamu, ni kundi la Mungu.

YESU NDIYE MCHUNGAJI WA KWELI
Yohana 10:11 "***Mimi ndimi mchungaji mwema. Mchungaji mwema huutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo."***
Mchungaji wa kweli ameandalika **kuyatoa maisha yake kwa ajili ya kondoo, anawachunga na kuwalinda.** Hili ndilo jukumu la mchungaji, kuwaongoza watu kwa uhusiano wa kibinafsi na mchungaji mkuu mwenyewe. Sisi ni wanakondoo wa Mungu sio kondoo wa mchungaji. Yesu ndiye mchungaji mkuu wa kanisa lake. Wanakondoo ni wa Mungu. Jukumu la huduma ya mchungaji ni kuwahusisha vyema watu wa Mungu na Bwana, ili watu wasikie sauti na waongozwe naye.

Wito wa huduma una gharama kuu
Katika **Yahona 10:8-11** Yesu anasema kwamba wale wanaoingia kwa mlango watapata malisho na watapata uzima, kondoo wakimjia watakuwa salama. Mchungaji mwema "***hutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo."*** **Mchungaji lazima awe tayari kutoa uhai wake kwa watu wa Mungu.** Kila mtu apokeaye wito huu, ni kwa msingi kwamba maisha yako sio yako tena. Wachungaji wote ambao kwa hakika wameitwa na kupewa karama na Mungu wako chini ya mchungaji Yesu.
Mchungaji wa kweli anaufuata mfano wa Yesu: -
Atawapatia kondoo chakula, akihakikisha kwamba wamelishwa vyema na neno ili wawe na uhai wa kukua
Atalilinda kundi na kuwa tayari kuutoa uhai wake kwa ajili ya kondoo.

YESU NDIYE MLANGO WA KONDOO
Yohana 10:7 ***"Basi Yesu aliwaambia tena, Amin, amin nawaambieni, Mimi ndimi mlango wa kondoo.'''*** Kondoo wanatakiwa kujua sauti ya mchungaji, [**Yohana 10:3].**
Ambaye sio mchungaji wa kweli hatashughulikiwa kondoo vilivyo [**Yohana 10:12-13].** Mtu wa aina hiyo ni wakulipwa ambaye hawezi kusimama juu ya mashambulizi ya adui, lakini wanaruhusu nyangau/ mbwa mwitu kularua kundi. **Mchungaji huwalinda watu wa Mungu kutokana na yule muovu.** Yeye huomba ua la ulinzi kwa kondoo.
Mchungaji wa kweli hawavuti wanafunzi kwake lakini huhusisha kila mtu kwa Yesu.
YESU ANA KONDOO WENGINE WASIO WA ZIZI LAKE
Yesu pia alionyesha kuhusika na kundi wengine walio nje ya zizi **[aya16}.** Hii inaonyesha moyo wa uinjilisti katika mchungaji. Kuna wengine wengi wanataka kuokoka. Mojawapo wa mitego ya wachungaji ni kushughulikia tu jamii ya waliookoka, wakisahau waliopotea

ONO LA YEREMIA KWA KUNDI LA MUNGU

Bwana ameahidi kutakua na zizi lenye usalama [mahali pa kudumu] kwa watu wa Mungu, ambapo pana afya na uponyaji, amani na kweli, urejesho na kusafishwa kutoka kwa dhambi.

Muite Bwana

Katika **Yeremia 33:3** BWANA asema ***"Niite, nami nitakuitika, nami nitakuonyesha mambo makubwa, magumu usiyoyajua".*** Kisha katika sehemu hio ingine ya mlango anatuambia mambo hayo ***'makubwa, magumu'***ni gani.

Afya na kupona

Aya 6 Mungu anasema mahali ambapo pamekuwa na nyumba zilizobomolewa, mahali ambapo pamekuwa na kifo na uharibifu **(aya 4 na aya 5), Ataleta afya na kupona**. Ataenda kuleta ***"afya na kupona, nami nitawaponya; nami nitawafunulia wingi wa amani na kweli"***

Urejesho

Aya 7 Mungu asema ijapo uharibifu unakuja, **Atarejesha**.

Kutakasa na kusamehe

Aya 8 ***"Nami nitawasafisha na uovu wao wote, ambao kwa huo wamenitenda dhambi; nami nitawasamehe maovu yao yote, ambayo kwayo wamenitenda dhambi, na kukosa juu yangu."***

Furaha, sifa na heshima; wema na ufanisi

Aya 9 Mahali ambapo pamekuwa ukiwa na sasa pameponywa na pamerejeshwa patakuwa mahali pa furaha, na sifa na heshima. Patakuwa mahali pa wema na ufanisi.
Aya 10 ***"…katika miji ya Yuda (sifa), na katika njia za Yerusalemu (amani)…"*** nini kitasikika?

Sauti za Harusi

Aya 11 "***Itasikilikana tena sauti ya furaha na sauti ya shangwe, sauti ya bwana arusi na sauti ya bibi arusi, sauti yao wasemao, Mshukuruni BWANA wa majeshi, maana BWANA ni mwema, rehema zake ni za milele."***

Mahali salama pa watu wa Mungu

Aya 12 BWANA amefanya kazi ya ajabu ya urejesho, na kisha anasema kwamba**.**
"*Yatakuwepo makao ya wachungaji wakizilaza kondoo zao"*
Mchungaji wa kweli ataruhusu tu kundi lilazwe chini mahali pa amani na usalama.

Kila mmoja anajulikana na Bwana

Aya 13 ***"…makundi ya kondoo yatapita tena chini ya mikono yake awahesabuye, asema BWANA."*** Ni Yesu ahesabuye kundi lake, anajua kama mmoja amepotea.

BWANA atasababisha aje haya yote aliyoahidi yatendeke?

Aya 14-15 ***"Katika siku zile, na wakati ule, nitamchipushia Daudi chipukizi la haki; naye atafanya hukumu na haki katika nchi hii. Katika siku zile Yuda ataokolewa, na Yerusalemu utakaa salama; na jina lake atakaloitwa ni hili, BWANA NI HAKI YETU"***
Kanisa hili lenye utukufu ambalo litainuka litaitwa kwa jina lile lile kama la mmewe, **YHWH TSIDKENU** [**BWANA HAKI YETU]!**
Kanisa hili lenye utukufu linaumbika katika ushirika ulio salama, ambao unainuka katika kila mahali katika dunia yote, ambapo watu wanaachana na tamaduni za watu na kumrejelea Bwana kupitia neno lake na nguvu za Roho Mtakatifu.

WACHUNGAJI NI AKINA NANI NA JUKUMU LA WACHUNGAJI NI LIPI?

Neno **'mchungaji'** linapatikana mara moja katika Agano jipya katika **Waefeso 4:11**. Ni huduma ya kupaa iliyopeanwa na BWANA Yesu aliyepaa kwa kanisa kusudi kulileta kanisa

katika ukomavu. Huduma zote tano ni sehemu ya BWANA Yesu anapatiana kwa watu kwa kusudi ya huduma kwa kulileta kanisa lake kwa utukufu mkamilifu.
Ili kuelewa huduma ya 'mchungaji' tunatakiwa kuangalia jukumu la 'mzee' katika maandiko.
Maagizo yaliopeanwa kwa wazee katika maandiko inathihirisha kwamba huduma ya msingi ya mzee ni ile ya mchungaji.

WAZEE: JE NI WACHUNGAJI?
Kutajwa mara ya kwanza kwa **wazee** katika Agano Jipya, ni katika **Mdo 11:30** "***Wakafanya hivyo, wakawapelekea wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli."*** Kutajwa huku kwa wazee kunazungumzia ofisi ya mzee. Sio huduma tukisema [huduma zote tano ni wazee **1Pet 5:1].** Wakati ambapo huduma zote za upao ni za wazee, huduma ya mchungaji inaeleweka kwa kutazama maelekezo ya wazee katika Agano Jipya.

WAZEE WANATAKIWA KUPEANA UANGALIZI NA KUCHUNGA KUNDI LA MUNGU.
Waefeso 4:11 ***Wachungaji S.C.#4166, haijulikani chanzo, mchungaji (kimsingi) mlinzi, mchungaji.***
Vines: 'poimen' - mchungaji, ambaye, anashughulikia kundi [sana sana sio yule anazipatia chakula] inatumika kwa mafumbo kuhusu muangalizi wa kikristo. Mchungaji anaelekeza na pia huwalisha kundi. 'poimaino' kama katika Yohana.21:15,17 na 1 Petro 5:2

Katika **Mdo 15:6** tunawaona mitume na wazee katika kanisa katika Yerusalemu wakija pamoja kuliangalia jambo. Sio wazi katika maandiko kama wazee haswa ni kati ya karama ya huduma ya upao lakini ni wazi kwamba wana wajibu wa uongozi wa juu. Katika **aya 13 Yakobo** ndugu ya Yesu, ni **mzee kiongozi wa kanisa.** Kama mtume **[Wagalatia 1:19],** anaongea na mamlaka katika jambo la imani na utendaji. Yakobo ana neno la hukumu/ubabanuzi. Pengine katika hali hii, Yakobo ni mtume akifanya kazi kama mchungaji kiongozi ama jukumu la mzee mwelekezi katika Kanisa kuu Yerusalemu.

WAANGALIZI NA WACHUNGAJI
Katika **Mdo 20:17** Tunasoma kuhusu Paulo akiwaita wazee wa kanisa katika Efeso akiwapa motisha na himizo. Katika **aya 28** anasema, "***jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake mpate kulilisha kanisa lake Mungu, alilolinunua kwa damu yake mwenyewe."***
Paulo anawahimiza wazee hawa '**kulilisha kundi'.** Kwa hivyo **wazee ni wachungaji.**
Roho Mtakatifu amewaweka kuwa waangalizi.
Huduma ya mchungaji ni kuliangalia kundi na ni uchaguzi wa Roho Mtakatifu.

Maaskofu ni waangalizi
Wazee wanatakiwa kutumika kama waangalizi na kulichunga kundi la Mungu. Katika maandiko maneno 'askofu' na 'wazee' yanatumika sawa. 'Askofu' yamaanisha 'waangalizi'.
Tito 1:5 ***"…na kuweka wazee kwa kila mji…"***
Aya 7 ***"Maana imempasa askofu awe mtu asiyeshitakiwa neno…"***
Maaskofu/wazee ni wachungaji
Ndio wale ambao wanatakiwa kuangalia na kuchunga kundi la Mungu.
Katika **1 Timotheo 3:1-7** tunasoma **maalekezo ya maasikofu: -**

Awe mtu asiyelaumika	mme wa mke mmoja
Mwenye kiasi	mwenye busara
Mtu wa utaratibu	mkaribishaji
Ajuaye kufundisha	si mtu wa kuzoelea ulevi
Si mpiga watu	asiwe mwenye kupenda fedha

Mpole Asiye na tamaa yake	si mtu wa kujadiliana mwenye kuisimamia nyumba vyema

Aya 7 "***Tena imempasa kushuhudiwa mema na watu walio nje; ili asianguke katika lawama na mtego wa Ibilisi"***

1 Petro 5:1-4 ***"Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa utukufu utakaofunuliwa baadaye; lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa, bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. Na mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka"***

Mtume Petro anadhibitisha maagizo ya Paulo:

1. Wazee wanatakiwa kulilinda kundi la Mungu;
2. Wazee wanatakiwa kuwa waangalizi;
3. Wazee wanatakiwa kuwa vielelezo kwa kundi.

WACHUNGAJI WANALIELEKEZA NA KULILISHA KUNDI

Hii ni huduma ambayo ni ya kuelekeza na kulisha kundi. **Yohana 21:15-17** inafundisha kundi linastahili 'kulishwa' na 'kulindwa'. Kuna maneno mawili ya Kiyunani yanayo tumika hapa, ambayo yote yametafsiriwa kama neno 'lisha' katika K.J.V.

Aya 15 ***"Lisha wanakondoo."***

S.C.#1006 *Bosko,* kulisha, kupea chakula, kulisha kwa zizi, kupatia mtu kitu cha kula, hali ya kupatia msaada kwa mtu.

Hii ni huduma ya kulisha kondoo: kukuza na kufanya wanafunzi.

Aya 16 ***"Chunga kondoo zangu".***

SC.# 4165 *Poimaino,* kuchunga kama mchungaji, kwa mafumbo kuchunga ni kuwa mwangalizi: - jukumu la kulisha (mifugo).

Hii ndio huduma ya uangalizi, kutoa maelekezo, kuelekeza kwenye malisho yenye usalama, na kupatiana mahali pa kujilaza.

Petro **kama mtume anaitwa na Yesu awe 'mchungaji' wa kandoo wake.** Huduma ya kweli ya Kristo lazima kuongoza kwa mfano. Yesu aliongoza kwa mfano. Yeye ndiye mchungaji mwema na aliutoa uhai wake kwa sababu ya kondoo. Wale walio wachungaji wazuri wa kondoo watapokea dhawabu kutoka kwa mchugaji mkuu.

YESU ANATAWALA KAMA MFALME MCHUNGAJI

Ufunuo 2:27 ***"Yeye atawachunga kwa fimbo ya chuma…"*** Neno tawala katika aya hii ni sawa na neno la Kiyunani *Poimaino* – kulinda kama mchungaji, mwangalizi. Njia ambayo Yesu anatawala kama mchungaji.

Ufunuo. 19:15 "…*na atawachunga kwa fimbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu Mwenyezi".* Tena neno chunga inamaanisha kama kuchunga kundi la Mungu. **Yesu anachunga kama Mfalme Mchungaji.**

MWANGALIZI NI LAZIMA ATOE HESABU

Waebrania 13:17a inazungumzia njia nyingine ya huduma ya mchungaji, "***Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea, maana hao wanakesha kwa ajili ya roho zenu, kama watu watakaotoa hesabu".***

Huduma ya uangalizi ya **Mchungaji ni kuangalia mioyo yenu na kutoa hesabu kwa Bwana.**

Wachungaji watawajibika kwa Mungu kwa jinzi walivyo angalia kondoo.

WANAWAKE WANAWEZA KUWA WAZEE?

Katika **Mdo 18:26** Prisila anatajwa akifanya **huduma 'ya kufundisha'** pamoja na mmewe, yeye ni 'msaidizi' ama '**mjori'/mfanyi kazi mwenza** na Pulo **(Warumi 16:3)** na kanisa katika Korintho walikutana kwa nyumba yake **(1Wakorintho16:19)**.

Mtume Yohana anaandika "***kwa mama mteule"*** katika **2 Yohana.** Barua inasoma kama iliyoandikiwa mtu mwenye 'mamlaka ya uangalizi' katika nyumba ya Mungu. Ana wana wa kiroho.

'Yunia' ambaye vile vile ingekuwa jina ya mwanamke, anatajwa katika **Warumi 16:17** kama mtume.

Katika **Warumi 16:1** Paulo anampongeza Fibi na kulihimiza kanisa la Mungu kumpa msaada wote anaohitaji ili afanikishe huduma yake. **Yeye ni mhuduma kanisani.**

WAZEE NI AKINA NANI NA NI NINI KINGINE WANATENDA?

1. **Wazee ndio watu wanaoongoza**

SC. Kiyunani#4244 Uzee[presbuterion] – mwili wa wazee (hakika wazee wenye makamu) Wakiwemo watu wenye heshima, hekima na ukomavu.

2. **Wazee wanaweza kuekeza/kuachilia karama**

1 Timotheo 4:14 Paulo anasema kwa Timotheo, "*Usiache kuitumia karama iliyomo ndani yako, uliyopewa kwa unabii, na kwa kuwekewa mikono ya wazee.*

Timotheo alikuwa amewekwa wakfu na wazee/wachungaji kupitia kuwekewa mikono.

3. **Wazee wanahusisha karama zote za kupaa**

Wazee waliomweka Timotheo wakfu alikuwemo Paulo. Mitume wote, manabii, wainjilisti, na waalimu na pia wazee. Kila mmoja wa hawa anaweza kuhudumu kama mchungaji. **Mdo 13:1-4** wazee walikuwemo manabii na waalimu.

4. **Wazee wanatakiwa kufundisha neno**

1 Timotheo 5:17. "*Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha".*

TAMATI.

Haijabainika wazi katika Agano jipya jinsi huduma tano zilifanya kazi. Kanisa la wakati huu limekosolewa kwa kuwa na karama moja inayo tamalaki ya wachungaji kadhaa, waalimu wachache, mara kwa mara wainjilisti katika huduma ya wakati wote, wakati mwingine nabii na mara kidogo mtume.

Katika Agano Jipya mitume na manabii walitembea kutoka mahali pamoja hadi pengine, na kutoka kanisa hadi lingine. Mwinjilisti naye alikuwa akienda hapa na pale, ijapokuwa Filipo alikuwa na kanisa la nyumbani kule Kaisaria **(Mdo 21:8).** Mchungaji na mwalimu walikuwa kanisa la nyumbani. Hakuna ushahidi wa wachungaji na waalimu ambao walikuwa wakisafiri.

Katika **Mdo 13:1** inaonekana wazee (Wachungaji) wa kanisa la Antiokia walikuwa manabii na waalimu waliojulikana. Tukichimbua Agano Jipya kikamilifu, tukitafuta huduma ya mchungaji, tunaona wazee walitakiwa wawekwe kwa kila mji **(Tito1:5)**

Hawa ni wale waliochaghuliwa na kupewa karama (kupakwa), kuhudumu kama wachungaji, kwa mfano, wakiwa waangalizi na wachungaji (wakilisha na kutunza) kundi la Mungu.

Kama mtume anakaa katika kanisa la mahali pamoja na anaangalia na kuchunga kundi, yeye kisawa anaitwa mchungaji kwa maana hiyo ndiyo huduma anafanya. Hayo yanatendeka pia kwa mwinjilisti, mwalimu ama nabii kama amekaa kwa kanisa la mahali pamoja akifanya huduma ya mzee. Kwa hivyo inaeleweka na kukubalika kanisani kuwa na mchungaji haswa. Hao ndio wamepewa wajibu wa kuangalia na kuchunga kundi la Mungu. Hata hivyo, mabadiliko yanayo hitajika kuja ni kwa kuzitambua huduma zile zingine nne za upao mtume, nabii, mwinjilisti, na mwalimu.

SURA YA SITA:

KARAMA YA HUDUMA YA MWALIMU

Waefeso 4:11 ***"Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu"***

Mwalimu

YESU MWALIMU.

Ili tuelewe huduma ya mwalimu tunatakiwa kuangalia mifano ya Yesu. Alijiita 'mwalimu'na alitambuliwa kama 'Mwalimu' na wengine

Katika Mathayo 23:8 "*Bali ninyi msiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu."* Aya 10 *"Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja, naye ndiye Kristo."*

Huduma ya mwalimu ni karama ya huduma ya upao ya BWANA ndani yetu.

1. **Mtazamo wa kwanza katika huduma ya mchungaji ni lile jukumu la mtumishi. Jambo** moja lijulikanalo alilolitenda Yesu ni kuwatawadha miguu wanafunzi Wake.**Yohana 13:13-14:** Yesu alisema "***Ninyi mwaniita, mwalimu, na, Bwana; nanyi mwenena vema, maana ndivyo nilivyo. Basi ikiwa mimi, niliye Bwana na mwalimu, nimewatawadha miguu, imewapasa vivyo kutawadhana miguu ninyi kwa ninyi"***

2. **Mtazamo wa pili wa huduma ya mwalimu: ushahidi wa ishara na maajabu zikiambata na huduma.**
   Katika **Mariko 10:17** yule kijana tajiri mtawal alitambua kwamba Yesu ni mwalimu, "***Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio, akampigia magoti, akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?"'***
   Nikodemo, mkuu wa Wayahudi, pia alitambua Yesu kama mwalimu. ***Yohana 3:2. "Huyo alimjia usiku, akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa wewe u mwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye."***

3. **Yesu aliye mwalimu aliwafundisha wanafunzi wake: Tunatakiwa kuwafundisha wanafunzi neno la Mungu.**
   Mathayo 5:2 ***"Akafumbua kinyua chake, akawafundisha"***

4. **Pia alifundisha katika Sinagogi: huduma ya kufundisha ni ya waliookoka,**
   Mathayo 4:23 ***"Naye alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akifundisha katika Masinagogi yao, na kuihubiri Habari Njema ya ufalme, na kuponya ugonjwa na udhaifu wa kila namna katika watu"***
   Huduma ya kufundisha ni kwa waliookoka, katika kanisa; huduma ya kuhubiri ni kwa wale waliopotea, ikileta ujumbe wa wokovu.

MUNGU AMEWEKA WAALIMU KANISANI

Katika **Mathayo 28:19-20** yesu aliwaagiza wanafunzi wake "***Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa njina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari."***

Kufanya wanafunzi
Huduma ya kanisa ni kufanya wanafunzi '***fanya wanafunzi kwa mataifa yote'***, kwanza ***'kuwabatiza kwa jina',*** Huu ni uinjilisti kwa maana ni waumini tu wanaobatizwa;
pili '**mkiwafundisha kuyashika yote.'** Wanafunzi wanatakiwa kufundishwa neno la Mungu. Yesu ndiye **'mwalimu';** anatuamuru tufundishe "***mambo yote niliyowaamuru".*** Huduma ya mwalimu ndiyo ya maana sana kanisani. Bila kufundishwa neno la Mungu, kanisa haliwezi kuufikilia utimilifu.

Mungu ameweka huduma ya kufundisha kanisani.
1 Wakorintho 12.28 "*Na Mungu ameweka wengine katika Kanisa, wa kwanza mitume, wa pili manabii, wa tatu waalimu, kisha miujiza, kisha karama za koponya wagonjwa, na masaidiano, na maongozi, na aina za lugha."*

WALIMU KATIKA KILA HALI YA MAISHA
Waalimu ni mojawapo wa karama zilizoandikwa katika **Warumi 12:6-8.** Mungu Baba amepeana karama ya **'waalimu'** kwa uzao wa mwanadamu. Mafundisho ni ya muhimu katika kila hali ya mwanadamu katika maisha, sio tu katika injili.

KARAMA YA HUDUMA YA MWALIMU
Mungu ameweka waalimu katika mwili wa Kristo hata kama vile Mungu aliweka mitume na karama hizo zingine zote.
Paulo ni mtume, lakini anajitambua pia kama mwalimu aliyechaghuliwa na Mungu.
Katika Mdo 13:1 tunaambiwa kwamba kulikuwa na manabii na waalimu katika kanisa la Antiokia.
Paulo alikuwa miongoni mwa hawa kwa hivyo alikuwa akihudumu kama mwalimu katika kanisa la Antiokia.
Katika **1 Timotheo 2:7** Paulo anasema kujihusu ***"…niliwekwa niwe mhubiri na mtume, (nasema kweli, sisemi uongo), mwalimu wa Mataifa katika imani na kweli."***
Paulo alikuwa mhubiri [mwinjilisti], mtume [mjenzi wa kanisa], na mwalimu. Alifundisha imani, alifundisha kweli na alichaghuliwa na Mungu kufanya hayo.
2 Timotheo 1:11 "***Ambayo kwa ajili ya hiyo naliwekwa niwe mhubiri na mtume na mwalimu".*** Paulo alikuwa na karama tatu za huduma tano zilizoachiliwa kwake.

Kuna hali ya kitume katika huduma ya mwalimu.
Paulo kama mtume pia ni mwalimu. Ni fundisho la mitume ambayo inaweka msingi wa imani na inafunua hekima ya ndani kwa kanisa.

NI NINI KINATAKIWA KUFUNDISHWA?

1. **Mwalimu anatakiwa afundishe njia za Mungu na afundishe kwa kweli.**

Katika **Mathayo 22:16** Tunasoma kile ambacho Mafarisayo walimwambia Yesu ***"…Mwalimu, twajua ya kuwa wewe u mtu wa kweli, na njia ya Mungu waifundisha katika kweli…".***

2. **Mwalimu anatakiwa kufundisha ambacho BWANA amemuamuru afundishe.**

Yesu alisema katika **Mathayo 28:20,** wakati alikuwa akipatiana lile tume kuu kwa wanafunzi wake**, "*na kuwafundisha kuyashika yale yote niliyowaamuru ninyi."***

3. **Fundisho la mitume linapaswa kufundishwa.** Waumini wapya wanatakiwa kufundishwa kumhusu Yesu.

Katika **Mdo 2:42** kanisa la kwanza "***walikuwa wakiduma katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali."***

4. **Mwalimu anatakiwa kufundiha fundisho la kweli.**

Tito1:9 ***"Akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga"***

5. **Walimu wanatakiwa kuwa na uwezo wakuwafundisha waumini wapya misingi.**

Huduma ya mafundisho ni ya muhimu sana kwa kukua kwa kanisa kwamba muandishi wa **Waebrania** anatarajia waumini wote wawe waalimu kwa sehemu fulani. **Waebrania 5:12** ***"Kwa maana, iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu."***

Mafundisho ya kwanza yamenakiliwa katika **Waebrania 6:1-2** ***"…Msingi wa kuzitubia kazi zisizo na uhai, na wa kuwa na imani kwa Mungu, na wa mafundisho ya mabatizo, na kuwekea mikono, na kufufuliwa wafu, na hukumu ya milele".*** Hii ndiyo **'misingi'** ambayo inatakikana kufundishwa. Misingi hii inatakiwa kuimarishwa vyema katika maisha ya kila muumini ili aweze kuenenda mpaka ukomavu/utimilifu.

6. **Waalimu wanatakiwa kuongea na hakima ambayo imetoka kwa Mungu.**

1Wakorintho 2:6-7 ***"Walakini iko hekima tusemayo kati ya wakamilifu; ila si hekima ya dunia hii, wala ya hao wanaoitawala dunia hii, wanaobatilika, bali twanena hekima ya Mungu katika siri, ile hekima iliyofichwa, ambayo Mungu aliiazimu tangu milele, kwa utukufu wetu."***

HUDUMA YA KUFUNDISHA NI NINI?

Huduma ya kufundisha inahusisha **kuweka misingi katika maisha ya watu.** Misingi inatajwa katika **Waebrania 5:12** kama maziwa ya neno, lakini wakristo wanahitaji chakula kigumu.

Huduma ya kufundisha inajumuisha **kuwafundisha watu mambo ya ndani kumhusu Mungu,** ambayo inawawezesha kuenenda katika utimilifu, **Waebrania 6:1.** Wanahitaji kusikia neno la haki, (**Waebrania 5:13).** Ni neno la haki litakalo wawezesha waumini kukua hata ukomavu.

Waalimu wanafundisha neno la Mungu: neno lina nguvu kwa sababu linahukumu mioyo.

Hili ndilo neno lililonenwa katika **Waebrania 4:12** ***"Maana neno la Mungu li hai, tena lina ngvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."***

Mtu anayekaa katika **neno la haki na anapokea hekima ya ndani ya maarifa ya Mungu** hatandanganywa, lakini hukua katika maeneo yote katika Kristo aliye Kichwa **(Waefeso 4:14)**

Kazi ya huduma ya kufundisha

Mtume Paulo anatuambia bayana ya kazi ya huduma ya kufundisha katika **Wakolosai 1:28-29,** ***"Ambaye sisi tunamhubiri habari zake, tukimwonya kila mtu, na kumfundisha kila mtu katika hekima yote, tupate kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo. Nami najitaabisha kwa neno lilo hilo, nikijitahidi kwa kadiri ya kutenda kazi kwake atendaye kazi ndani yangu kwa nguvu"***

1. **Tunapaswa kuhubiri Kristo**
2. **Tunapaswa kumwonya kila mtu katika hekima yote**

Katika **Waefeso 3:8** Paulo anazungumzia kuhubiri '***utajiri wa Kristo usiopimika'.***
Wakolosai 2:3 inatuambia kwamba katika Kristo ***'hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika'***
Ni jukumu la mwalimu kutafuta maarifa yaliyofichwa na kuwapokeza wengine.
Hekima na maarifa zimefichwa ndani ya Yesu Kristo. Huwa zinafunuliwa kwa kujitoa katika kujifundisha neno na kulifungua neno la Mungu.

WAZEE WANATAKIWA KUFUNDISHA
1Timotheo 3:2 "*Askofu awe mtu ... ajuaye kufundisha"*
1Timotheo 5:17 *"Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu; hasa wao wajitaabishao kwa kuhutubu na kufundisha".*

ONYO KWA WAALIMU WA UONGO

2 Timotheo 4:3-4 "*Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo".*
2 Petro 2:1 *"Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia".*
Uzushi wa kupoteza ni yale mambo yaletayo migawanyiko. Twahitaji kujihadhari na waalimu wa uongo ambao wanafundisha mafundisho ya uongo.

UPAKO UTATUFUNDISHA MAMBO YOTE NA HAUTASEMA UONGO
Yohana anatuambia **upako unaokaa ndani yetu ambao Mungu anampa kila mtu ni upako ufundishao na Roho Mtakatifu ndani yetu kila mara atashuhudia kwa ile kweli (1Yohana 2:20 na 27).**

WAALIMU WATAHESABIKA KWA MUNGU KWA YALE WANAYOYAFUNDISHA
Yakobo 3:1 *"Ndugu zangu, msiwe waalimu wengi, mkijua ya kuwa tutapata hukumu kubwa zaidi."*

TAMATI

Karama ya huduma ya mwalimu ni ya msingi na yale yote yanayohusika na maisha ya kanisa. Katika aya za kumalizia kitabu cha **Mdo 28:30-31** tunasoma kumhusu mtume Paulo,
"***Akakaa muda wa miaka miwili mizima katika nyumba yake aliyokuwa ameipanga, akawakaribisha watu wote wliokuwa wakimwendea, akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu."***
Paulo alikuwa na karama ya huduma ya 'mwalimu'. Katika kutajwa mara ya mwisho katika kitabu cha Matendo ya mitume anaendelesha huduma ya waalimu ambayo alipewa na Mungu. Kote ambapo neno la Mungu limefundishwa kwa uaminifu kutakuwa na wanafunzi waliofaulu wakiinuliwa kusongesha injili. Himizo nyakati zetu ni urejesho wa mafundisho ya mitume kanisani. Mafundisho ya mitume yanapopokelewa tena huduma ya waalimu itarejeshwa kikamilifu na kuachiliwa. "***Hizi ndizo huduma za waalimu ambazo zina maji yaliyo hai – ukweli uletao uzima****." [Rick Joyner, p.62, jarida ya nyota ya asubuhi Vol. 11, No.4]* Nabii Habakuki aliiona kwa njia hii, "***Kwa maana dunia itajazwa maarifa ya utukufu wa BWANA, kama maji yaifunikavyo bahari"* (Habakuki 2:14).**

SURA YA SABA:

NEEMA YA KUKUA HADI UKOMAVU
WAEFESO 4:7-16

LENGO NI UKOMAVU (UTIMILIFU)
Lengo la Mungu kwa kanisa la Yesu Kristo ni kwa kanisa likue hadi ukomavu; kutakuwa na kanisa lenye utukufu bila ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo kama ifaavyo uhusiano wa milele na Mwana wa Mungu! **Waefeso 4:7-16** ndiyo sehemu tu katika Biblia ambapo huduma tano zimeelezewa. Ni katika mazigira haya ambao tunapata kwamba neema inapeanwa kwa kila mshirika wa mwili wa Kristo kupitia huduma ya mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu kuwezesha mushirika na hivyo mwili wote kukua hadi ukomavu.

NEEMA HUJA KUPITIA KILA KIPAWA CHA HUDUMA
Waefeso 4:7 "*Lakini kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo*".
Kipawa ni huduma tano ya mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji na waalimu waliopeanwa kanisani na Bwana aliyepaa. Kupitia kila huduma hizi neema huachiliwa kanisani kwa mwili wa Kristo. Kama moja yapo ya huduma hizi haijaachiliwa na kufanya kazi hivyo mwili wa Kristo haupokei neema yote ambayo inahitajika ili kukua mpaka ukomavu.

YESU KRISTO NDIYE KIPAWA CHA HUDUMA TANO
Mahali pengine tumeonyesha kutoka maandiko kwamba **Yesu mwenyewe ndiye mwaakilishi wa kipawa cha huduma tano:**
Yeye ni **mtume wa Mungu,** aliyetumwa na Mungu kulijenga kanisa;
Yesu ndiye **Nabii** aliyeinuliwa na Mungu kutoka miongoni mwa ndugu za Musa (**Kumbukumbu la torati 18:18)** kuyanena maneno ya Mungu;
Yesu ndiye **Mwinjilisti** aliyekuja kutafuta na kuwaokoa waliopotea, na kutoa uhai wake kama fidia kwa wengi;
Yesu ndiye **Mchungaji**, mchungaji mwema wa kondoo;
Yesu ndiye **Mwalimu,** aliyetoka kwa Mungu aliyefundisha kama aliye na mamlaka.

YESU ALITEKA MATEKA
Waefeso 4:8-10 inatuonyesha ya kwamba Yesu alipopaa juu, aliwateka mateka wa kuzimu na ibilisi mateka, na kupeana vipawa hivi kwa wanadamu. Kuyafikia matokeo haya ya kushangaza ilkuwa ni vyema kwa Yesu '***kushuka'*** mpaka pande zilizo chini za nchi**, akisukumia ushindi wa msalaba kwa ibilisi na mateka wa kuzimu.** Hivi ndivyo alivyowateka mateka. Sehemu kubwa ya nyara ambayo Yesu alipata kupitia ushindi wake juu ya shetani na kuzimu ni kuachilia kwa vipawa vya huduma tano kwa kanisa, hivyo akiwezesha kazi za huduma kufanya kazi, zikilileta kanisa kwa ukomavu. Mungu alikuwa amemuahidi Yesu dhawabu kuu katika **Isaya 53:12** kwa kuwa alizibeba dhambi zetu. Lakuhuzunisha ni kwamba kanisa lina ufahamu mdogo wa kuwa kupeanwa kwa huduma tano ilikuwa ya gharama kubwa kwa Bwana wetu na ni ya muhimu sana na ya maana katika kutimiza kwa makusudi yake.

KUSUDI LA MUNGU LA MILELE
Katika kitabu cha Waefeso na pengine Paulo anazungumzia **siri ambazo zimefunuliwa (Waefeso 3:3-4,9**) Na anazungumzia **kusudi la milele la Mungu ambayo alikamilisha**

katika Kristo Yesu Bwana wetu (Waefeso 3:11). Tunatakiwa kuelewa kwamba Mungu anafuatilia kusudi lake la milele. Hajayumba yumba kutoka kwa kusudi lake ambalo aliumba ulimwengu na kwa ambalo alituumba sisi wanadamu kwa mfano na sura yake. Vyote ambavyo vilikuwa vimepotea katika Adamu wa kwanza kupitia dhambi zimerejeshwa na Bwana wetu Yesu Kristo.
Kulingana na fundisho la Paulo katika **Waefeso 4, vipawa vya mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji na mwalimu zilitapikana tena wakati Yesu aliteka mateka wa kuzimu.** Ni wakati huo Yesu alipeana vipawa hizi kwa watu. Inawezekana kuona vipawa hivi vikiwa ndani ya Adamu wa kwanza, lakini zilitekwa kupitia dhambi ya Adamu na kutii shetani. Mungu amekusudia wakati wote kwa kanisa lenye utukufu liumbike na liinuliwe duniani kwa mwanawe. Mungu kila wakati alipatiana kila kitu kusudi haya yatendeke lakini iligharimu kifo cha Yesu na kushuka kwake kusimu na kupaa kwake kwenye utukufu kuachilia kikamilifu ambapo kusudi la Mungu linaweza kujulikana.

YESU ANALIJENGA KANISA LAKE KUPITIA HUDUMA TANO

Yesu Kristo ndiye jiwe kuu la pembeni la kanisa, ambalo linawakilishwa kama jengo. Yeye ndiye jiwe la msingi, jiwe lililojaribiwa, jiwe la pembeni lenye dhamani, msingi ulio imara **(Isaya 28:16).** Sisi ndiye mawe yaliyo hai tunaojengwa juu yake kuweka ukuta wa hekalu ya Mungu katika Roho (**1Petro 2:5 na Waefeso 2:19-23).** Yesu amepeana huduma za mtume, nabii, mwinjilisti, mchungaji na mwalimu kuwezesha kazi ya jengo lake liendelee na kusudi la Mungu la milele litimizwe.

HUDUMA TANO ZINALETA KANISA KATIKA UTIMILIFU

MAKUSUDI MATATU YA HUDUMA TANO

Waefeso 4:12 "*kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe"*

1. KWA KUSUDI LA KUWAKAMILISHA WATAKATIFU

Huduma tano zinapatianwa kwa **kuwakamilisha watakatifu.**

> ***Kukamilisha,*** *katartismos* (kat- ar- tis- moss); **SC# 2677 Kiyunani**: kukamilisha, kutayarisha, kuandaa, kukamilisha, kutengeneza kikamilifu kwa huduma. Katika kiyunani asili maneno yaliotumika ya kuweka mifupa vizuri wakati wa upasuaji. Tabibu mkuu sasa anafanya merekebisho yote ili kanisa lisiwe nje ya kiungo'.
> ***{Utajiri wa neno, S.F.L.B. p.1793}***

Makusudi ya Mungu kwa kila mshirika wa mwili wa Kristo ni kukamilishwa kwa sababu ya huduma. Hakika sio wote wamewekewa kuwa katika huduma tano lakini kila mmoja ana wajibu spesheli wa kutimiza. Mpaka kila mtakatifu atakapoandaliwa kuhudumu mwili wa Kristo hautakua kufikia ukomavu.

2. KWA KAZI YA HUDUMA

Huduma tano imepeanwa **<u>kwa kazi ya huduma</u>:** kila mmoja kati ya huduma tano lazima afanye kazi. Sehemu kubwa ya kanisa haipokei neema ambayo imepatianwa na Yesu aliye Kiongozi wa kanisa, kwa sababu mitume, na mara kwa mara sehemu ya huduma zingine tano hawajapokelewa. Kama nimeitwa kuwa mtume na ninafanya kazi kama mchungaji tu katika kanisa la mahali pamoja basi sifanyi kazi ya huduma ambayo nimeitwa kufanya. Mojawapo wa urejesho wa ajabu ambao unatendeka kote katika mwili wa Kristo duniani kote ni kwamba watakatifu wanaachiliwa katika huduma kwa sababu **Yesu anawainua mitume na kuwatuma kuifanya kazi ya huduma.** Pia watu ambao wanaendelea kufanya kazi ya huduma wanaingia katika huduma tano kwa ujasili kama Roho Mtakatifu anaita na kutenga watu fulani kwa huduma hizi. Hii imeonyeshwa vyema katika maisha ya mtume Paulo

ambaye alikuwa hajawekwa wakfu kuwa mtume mpaka **Mdo 13,** lakini alikuwa anaendelea kufanya kazi ya huduma kabla ya hayo.
Kazi kubwa ya huduma ni kuwakamilisha watakatifu na kisha kuwaachilia [kuwatuma]. Kwa mfano hivi punde kule Myanmar, ndugu ambaye ni mwinjilisti lakini alikuwa hajaachiliwa na mtume ama na mojawapo ya huduma tano, alikuwa anafikia nafsi nyingi lakini alikuwa hawabatizi kwa kuwa alikuwa anajihisi hana mamlaka kufanya hivyo. **Mojawapo ya kikundi chetu, wakifanya kazi ya utume, waliona hitaji la kufanya hivyo na wakamtuma.** Sasa ana ujasili wa kubatiza. Halleluyah!!

3. KUJENGA MWILI WA KRISTO

Huduma tano zinapatianwa **kwa kujenga mwili wa kristo:** Hivyo ni, kujenga mwili wa Kristo. Yesu aliahidi katika **Mathayo 16:18** ya kwamba analijenga kanisa. Analijenga kwa jinsi gani? Analijenga kanisa kupitia vipawa vya huduma tano ambavyo amepatiana. Ndiposa urejesho wa huduma tano ni wa muhimu katika kulitimiza kusudi la Mungu; kanisa lenye utukufu ambalo limekuwa hadi utimilifu halitajengwa bila kipawa cha huduma tano kurejeshwa kikamifu na kufanya kazi.

ISHARA ZA UKOMAVU

Waefeso 4:13 "*Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo"*

1. UMOJA WA IMANI

Kipimo cha kwanza cha ukomavu ni **umoja wa imani.** Hii inamaanisha tukubaliane kuhusu neno la Mungu. **Makubaliano kama hayo yana msingi katika kulipokea fundisho la mitume,** sio kuyashika mafundisho ya watu, ama mapokezi yoyote ya dini. Kanisa la kwanza lilidumu kwa kujitoa katika fundisho la mitume **(Mdo 2:42).** Petro anatuambia "***Hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu"* (2 Petro 1:20)**. La kuhuzunisha kanisa katika historia imegawanyika katika misingi ya viongozi fulani na mara fundisho hilo linafundishwa badala ya Maandiko. Himizo limekuwa yale yaliyosemwa na mtu babala ya kilichonenwa na Maandiko.

Umoja wa imani ni **ile** hali ya **kuishika sana neno aminifu ambalo umefundishwa.**
Ni kufuatilia fundisho la kweli katika mambo ya imani na utendaji.
Tito 1:9 *"Akilishika lile neno la imani vile vile kama alivyofundishwa, apate kuweza kuwaonya watu kwa mafundisho yenye uzima, na kuwashinda wenye kupinga".* Umoja wa imani ni kuwa na fundiso la kweli, vivyo ni, kuamini na kuishi kwa neno la Mungu.

Umoja wa imani ni hiyo imani (fundisho la mitume) "***Waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu"* (Yuda 3).** Mtume yuda anatuhimiza tuishindanie hiyo imani, **fundisho lililo peanwa na neno la Mungu kupitia mitume.** Kanisa la kwanza walijipatiana kwa fundisho la mitume. Kanisa la siku za mwisha litaufikia utimilifu kama tu fundisho la mitume litafundishwa na kupokelewa.

2. UFAHAMU WA MWANA WA MUNGU

Huu ni ufunuo wa ufahamu; kupokea ***"roho ya hekima na ya ufunuo katika kumjua yeye"* (Waefeso 1:17).** Hii inamaanisha kwamba Yesu ndiye wa muhimu kwa imani yetu na ujuzi, "***Awe mtangulizi katika yote"* (Wakolosai 1:18).** Paulo analia akisema, *"**ili nimjue yeye, na uweza wa kufufuka kwake*" (Wafilipi 3:10).** Petro anatufundisha hatua za kupata mazao katika "ufahamu wa Bwana wetu Yesu Kristo" **(2 Petro 1:8)** "***si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo".***
Hatua ni: "*katika imani yenu tieni…"*
Imani > wema >maarifa > kiasi > saburi > utauwa > upendano wa wandugu > upendo.

3. HATA KUWA MTU MKAMILIFU

Mwili wa Yesu unatakiwa kuwa mtu mkamilifu, **ukifananishwa na mfano wa mwana wake (Warumi 8:29); kulijua neno la haki (Waebrania 5:13). Tunatakiwa kumtazama Yesu mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu (Waebrania 12:2).**

4. KWENYE CHEO CHA KIMO CHA UTIMILIFU WA KRISTO

Tunatakiwa **tuwe kama Kristo, aliyepakwa, Mwana wa Mungu, ili awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi (Warumi 8:29).** Kanisa ni ukamilifu wake aliye kamilika kwa vyote katika vyote (**Waefeso 1:23).** Utukufu wa BWANA ndio utimilifu wa Kristo anapojaza kanisa lake.

5. TUSIWE TENA WATOTO WACHANGA…

Waefeso 4:14 ***"Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njia za udanganyifu".***

Ni wakati wa kukomaa, tukiishi kwa upako ambao tumepokea, ambao utatufundisha mambo yote wala hautandanganya (**1Yohana 2:20, 27).** Yesu alisema katika **Mathayo 24:5, "*Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ni Kristo; nao watandanganya wengi".*** Jihadhalini na waalimu wa uongo: wengi watakuja kwa mfano wa huduma ya Kikristo! Tunatakiwa kuwa wenye shina na wenye kujengwa katika yeye, mkifanywa imara kwa imani, msifanywe mateka kwa elimu ya wanadamu ya bure (**Wakolosai 2:6-8).** Tunatakiwa tuwe **imara na kuimarishwa kwenye Mwamba na kwa neno la Mungu. Mathayo 7:24-27** yatufundisha nini? **Tunastahili sote tumtazame Yesu, sio mtu yeyote, tukijenga kulingana na maagizo yake.**

6. TUSHIKE KWELI KATIKA UPENDO

Waefeso 4:15a "*Lakini tushike kweli katika upendo"*

Wanafunzi wanapokua katika utimilifu hawajihusishi na udaku ama masengenye; hawasunyi watu; bali hunena ukweli katika upendo! Kanisa linalokomaa ni watu wanaokuwa katika uhusiano. Ili uhusiano ukue katika Uungu na upendo wa kweli wa Kikristo, ukweli unatakiwa unenwe kwa upendo mmoja na mwingine. Hakuna nafasi ya kutafutiana makosa mmoja na mwingine. Endapo pana shinda kati ya wandugu na unashughulikiwa kulingana na mwelekeo wa maandiko, kisha upendo husitiri wingi wa dhambi **(1Petro 4:8).**

7. KUKUA HATA TUMFIKIE KRISTO KATIKA YOTE

Waefeso 4:15b "*Nakukua hata tumfikie yeye katika yote, yeye aliye kichwa – Kristo"*

Mkristo binafsi na kanisa kwa pamoja wanatakiwa kukua. Kila kitu katika maisha yetu kinatakiwa kufikia kiwango cha neno la Mungu wakati kazi ya neema inakamilishwa ndani yetu.

Tunatakiwa kupatikana ndani ya Kristo [aliyepakwa] pasina haki yetu, lakini tukiwa na haki ambayo hupatikana kwa njia ya imani ndani yake (**Wafilipi 3:9).** Kila kitu tufanyacho katika neno au matendo, tunatakiwa tufanye "***yote katika jina la BwanaYesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye"* (Wakolosai 3:17).**

8. UPENDO WA MUNGU UNAFUNULIWA KWA KANISA LILILOKOMAA

Waefeso 4:16 "*Katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na kushikamanishwa kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga mwenyewe katika upendo."*

Hii ni picha yenye nguvu ya kanisa lililokomaa; tambua tabia kuu ya kanisa lililokomaa ni UPENDO, aina ya upendo wa Mungu, wa kujitoa, wa kujipatiana! Kanisa lililokomaa limekomaa kwa sababu kila sehemu inafanya kazi kikamilifu, ikiungamanishwa na kushikamanishwa pamoja – umoja wa kweli! Kila sehemu na kila kiungo [katika mwili kiungo ni mahali ambapo viungo viwili vinaweza kushirikiana kikamilifu kufanya kazi]

unapatiana uhai na kila kiungo kinafanya kazi kwa kushikilia njengo lote. Uzima huu wote unatiririka kutoka kichwa, Bwana wetu Yesu Kristo.

SISI NI NYUMBA YA MUNGU

"*Sisi ndio nyumba ya Mungu"* (Waebrania 3:6) na Yesu Kristo ni MWANA juu ya nyumba ya Mungu. ***"Naye atalijenga hekalu la BWANA",* Zakaria 6:12.** *"**Alipopaa juu aliteka mateka, Akawapa wanadamu vipawa"*** **Waefeso 4:8.** Alipeana vipawa hivi **'kuujenga mwili wa kristo' Waefeso 4:12.**

Kanisa lazima lifikie ukomavu [utimilifu], ili liwe kielelezo cha utukufu wake duniani, "***Ili ulimwengu ujue wewe ndiwe uliyenituma"* Yohana 17:22-24*, Apate kujiletea kanisa tukufu, lisilo na ila wala kunyanzi wala lolote kama hayo; bali liwe takatifu bila mawaa".*** **Waefeso 5:27.** Mungu ana mawazo ya makusudi ya utukufu ya kanisa: Yeye ndiye mwili wa Kristo

Kupitia kanisa Mungu anataka kumfunua Mwana wake. Kusudi haya yatendeka kutakuwa na urejesho kamilifu wa huduma ya mitume pamoja na vipawa vyote vya huduma. Hii inatendeka katika siku zetu na inaharakishwa kwa sababu Mungu anakusudia kazi ya haraka ifanyike siku za mwisho **(Isaya 60:21-22).**

Moja ya jukumu kuu ya mtume kufanya kazi pamoja na nabii ni kuuweka msingi wa kanisa la Yesu **(Waefeso2:20).** Msingi kama huo unaachilia huduma zingine za mwinjilisti, mchungaji, na mwalimu kufanya kazi kikamilifu, na watakatifu wanahudumiwa vyema na kuinuliwa kufanya kazi katika mwili. Mtume anawajibika kwa fundisho [hiyo ni kufundisha neno la Mungu kwa usahihi] na kwa mikakati ya ujenzi. Paulo anasema alikuwa ni mjenzi mwenye hekima **(1 Wakorintho 3:10).** Mungu anawafunulia mitume jinsi ya kuweka msingi; wengine wanajenga juu yake. Nabii ana wajibu pamoja na mtume kupatiana msingi imara ndani ya Kristo kwa kuwaandaa na kuwakamilisha watakatifu, na kuinua huduma zingine.

NYUMBA YA MUNGU ITAJENGEKA!